# Nipashe

Jumanne Aprili 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581291

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



MID WEEK JACKPOT!


TZS. 560,305,280

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#

**Mwenyekiti** CCM ajinyonga madai kudhulumiwa mil. 118/- za kahawa

UKURASA 3


Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Kampuni digitali Korea Kusini yaingia ubia na Tume Tehama 'kusafisha' biashara nchini

'Mtale wa Ngariba', shairi lililompa Mwalimu Amri ushindi, na mamilioni

• Serikali rasmi yasambaza kazi yake shuleni

UKURASA 11

# Waziri aagiza uchunguzi madhara kuhusu 'energy'

UK. 2



Mwonekano wa daraja la Kigongo-Busisi linalojengwa mkoani Mwanza jana. Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, amesema ujenzi wa daraja hilo, umefikia asilimia 72 na ukikamilika utawezesha wananchi kuvuka kwa dakika nne badala ya saa mbili hadi nne walizokuwa wanatumia awali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RIPOTI UCHUNGUZI:

# Uhai wa Hifadhi Saadani shakani

UKURASA 4 & 5





Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi, Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam

Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com




# Serikali ilivyotatua kero sugu nne za Muungano

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAUTAKA UBINGWA SHIRIKISHO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Waziri aagiza uchunguzi madhara 'energy'

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameiagiza Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kufanya uchunguzi zaidi kuhusu matumizi ya vinywaji vyenye kuongeza nguvu (energy) ili kupata ushahidi wa kisayansi.

Ummy alitoa maagizo hayo jana kupitia mtandao wa kijamii wa 'twiter' na kuongeza kuwa uchunguzi huo ukifanyika utasaidia katika kukabiliana na tatizo hilo tofauti na ilivyo sasa ambapo chanzo cha kina hakijulikani ni nini.

Maagizo hayo yametolewa ikiwa ni siku moja baada ya gazeti hili kuchapisha habari ya kijana mwenye umri wa miaka 21 aliyefikishwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) akiwa na hali mbaya na baada ya uchunguzi kufanyika, ilibainika kuwa alizidisha matumizi ya kinywaji hicho.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kijana huyo alipokelewa katika taasisi hiyo akiwa na maumivu makali ya kifua upande wa kushoto ulipo moyo na kupewa huduma ya dharura.

Kwa mujibu wa Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo na Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Mafunzo JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, uchunguzi wa awali ulibaini kuwa kijana huyo hakuwa na magonjwa hatarishi yasiyoambukizwa kama moyo yanayosababishwa na ulevi, uvutaji sigara na uzito mkubwa.

Kutokana na hali hiyo, taasisi hiyo iliamua kufanya uchunguzi uliohusisha historia ya kijana na kubaini ni mtumiaji wa vinywaji vya kuongeza nguvu na kuwa kwa siku sita alikuwa amekunywa makopo matano kila moja likiwa na ujazo wa milimita 250.

Alisema, mgonjwa huyo alikuwa amekunywa lita moja na robo ya kinywaji hicho ndani ya saa nne na baada ya kumaliza kopo la mwisho, alipata maumivu makali upande wa kushoto na akaenda hospitalini.

Kwa mujibu wa Pallangyo, hali hiyo ilisababisha mishipa ya moyo kuziba, upande wa kushoto ukiziba kwa asilimia 100 na kwamba kama hali hiyo ingeendelea kwa saa kadhaa, misuli ya moyo ingekufa na hatimaye kukumbwa na kifo cha ghafla.

Baada ya kupatiwa matibabu ya dharura alipelekwa wodini huku akiwa amewekwa mrija kwenye eneo lililoziba na kutakiwa kutumia dawa kila siku kwa maisha yake yote.

# Serikali ilivyotatua kero sugu Muungano

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amesema mwaka 2022/23, ofisi yake iliratibu vikao vitatu vya kujadili masuala ya muungano, kwamba hoja nne kati ya nane zilizojadiliwa zilipatiwa ufumbuzi.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Ofisi ya makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/24, huku akiomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 54.

Jafo alizitaja hoja hizo ni malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; kodi ya mapato (PAYE) na kodi ya zuio; mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume; na ongezeko la gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO). Alisema, vikao hivyo vya kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), viliwashirikisha mawaziri na makatibu wakuu.

Waziri Jafo alisema hoja ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili ilitokana na kuwapo kwa utofauti wa ukadiriaji wa viwango vya thamani za bidhaa na kodi ya forodha baina ya Tanzania Bara na Zanzibar inayosababisha kulipa kodi ya ziada kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania Bara.

Alisema hali hiyo iliibua malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kwamba wanatozwa kodi mara mbili.

Jafo alisema ufumbuzi wa hoja hiyo ulipatikana baada ya kubainika kwamba wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa Zanzibar kutoka nje ya nchi na kupeleka Tanzania Bara, hulazimika kulipia tofauti ya kodi iliyoachwa kukusanywa Zanzibar kutokana na tofauti ya uthaminishaji wa bidhaa. Alisema suala hilo haliwafanyi wafanyabiashara kulipa kodi mara mbili badala yake hulipa kodi inayostahili kwa uthaminishaji uliofanyika Tanzania Bara. Alisema kwa sasa suala hilo linaeleweka vizuri kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

Kuhusu SMZ kutonufaika ipasavyo na PAYE ya wafanyakazi wa taasisi za Muungano walioko Zanzibar pamoja na kodi ya zuio itokanayo na kampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar, Jafo alisema: "Baada ya majadiliano, ufumbuzi wa hoja hii ulipatikana... hoja ya kodi ya zuio kwa kampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar, wizara zinazohusika na masuala ya fedha za SMT na SMZ, zilikubaliana kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 na Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 kupitia Sheria ya Fedha Namba 5 ya Mwaka 2022 ili kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara na zenye matawi Zanzibar kuweza kulipa kodi ya zuio Zanzibar.

"Kuhusu kodi ya mapato yatokanayo na mishahara ya watumishi wa taasisi za muungano zilizopo Zanzibar ufumbuzi uliopatikana ni kwamba Sh. bilioni 1.75 ambazo zilikuwa zikitolewa kwa SMZ kila mwezi kama malipo ya PAYE ziendelee kutolewa kwa SMZ."

Kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Jafo alisema hoja ilikuwa kuchelewa kutiwa saini kwa mkataba wa mkopo kati ya serikali na Benki ya Exim ya China baada ya mkataba kuhusisha vipengele vya kuweka mali za serikali kama dhamana ya mkopo. Alisema ufumbuzi ulipatikana baada ya SMT na Exim kukubaliana kuondoa sharti hilo, hivyo kuwezesha mkataba wa mkopo huo kusainiwa Novemba mwaka jana.

Kuhusu gharama ya umeme, Jafo alisema hoja ilikuwa kuongezeka kwa bei ya umeme kwa wateja wa TANESCO ikiwamo Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kulikotokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Alisema ongezeko hilo liliibua malalamiko kwa watumiaji wa umeme kwa upande wa Zanzibar na kwamba baada ya majadiliano, hoja hiyo ilipatiwa ufumbuzi kwamba mapendekezo ya ZECO kununua umeme kwa Sh. 130 kwa uniti yalikubaliwa.

Jafo alisema hoja nne zilizobaki za muungano zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi ni mgawanyo wa mapato yatokanayo na hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu.

Nyingine ni mapendekezo ya tume ya pamoja ya fedha; usajili wa vyombo vya moto na uingizaji wa sukari inayozalishwa Zanzibar katoka Tanzania Bara.

**WABUNGE WACHACHAMAA**

Baadhi ya Wabunge wameeleza kukerwa na hatua ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuendelea kutoza kodi bandarini kwa wananchi waliobeba bidhaa walizonunua kwa matumizi binafsi zikiwamo televisheni, sukari ili hali ni nchi moja.

Wakichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya makamu wa Rais, walisema hali hiyo imesababisha kinamama na kinababa wengi kudhalilika eneo la bandarini kwa kutokujua sheria na utaratibu wa kutakiwa kulipia kodi bidhaa walizonunua Zanzibar au Tanzania Bara, kuiomba serikali kuondoa utaratibu huo.

Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Bakar Hamad Bakar, akichangia bungeni, alimtaka Jafo aelezee sababu zinazofanya mwananchi kutozwa kodi pale anaponunua bidhaa kama televisheni kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara ilhali ni nchi moja.

"Haiwezekani mwananchi amesafiri kutoka Zanzibar amebeba kilo mbili za sukari, au televisheni moja iliyotumika ameinunua kwa ajili ya matumizi yake ya nyumbani anafika Tanzania Bara anaambiwa alipe kodi.

"Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzabnia ni nchi moja haiwezekani mtu anayetoka Morogoro kwenda Dar es Salaam halipi kodi, lakini anayetoka Zanzibar kuja Tanzania Bara akifika Dar es Salaam anatakiwa alipe kodi, hii ni kero kubwa, alisema mbunge huyo," alisema.

Kuhusu kero usajili wa magari alisema: "Tunaona magari ya nchi mbalimbali yanayozunguka hapa Tanzania hayaletewi usumbufu wowote lakini kuna tatizo kubwa kwa usajili na utambuzi wa magari yanayotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Tanzania ni moja kwa nini mpaka leo hakuna sheria inayosajili gari kutoka Zanzibar kutumika Tanzania Bara?"

Mbunge wa Magomeni , Mwanahamis Kassim, alisema alihoji hatua ya televisheni moja kulipiwa kodi wakati imenunuliwa ndani nchi moja. Alisema wanawake wengi ni wajasiriamali na wanafanyabiashara ndogo lakini wanakumbana na vikwazo vya kodi wanapofika bandarini wakiwa na mizigo yao.

Alisema, hali hiyo imewasababisha wengi kupoteza mizigo yao bandarini kwa kushindwa kuilipia kodi, huku wengine wakikata tamaa kufanya biashara Zanzibar- Tanzania Bara.

Akitolea ufafanuzi baadhi ya hoja zilizowasilishwa na wabunge, Waziri Jafo alisema ofisini yake bado inaendelea kuzitatua kero za muungano na kuwataka Watanzania kuwa wavumilivu.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI YA KUTOA HUDUMA NA VIFAA KUTHIBITI KUMWAGIKA KWA MAFUTA MAJINI/BAHARINI (TIER 2-10 M3)**

**KUMB: ETJ-BB-HS-EI-GEN-GE-0001**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, inatekeleza Huduma za Awali za ujenzi wa Gati na kituo cha kupakilia katika Ghuba ya Tanga kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

- Kutoa Huduma na Vifaa vya kuthibiti Kumwagika kwa Mafuta Baharini/Majini (Tier 2-10 M3).

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

- Nyenzo za kukabiliana na umwagikaji wa mafuta na vifaa vya kuthibiti kiwango cha kumwagika mafuta (Daraja la 2) -Kiasi ccha Lita 10,000 juu ya maji / baharini.
- Vifaa zilizoidhinishwa vya kushughulikia umwagikaji wa mafuta majini/ baharini wa Kiwango / Daraja la 2.
- Mafunzo kwa wafanyakazi wa mradi juu ya kushughulikia umwagikaji wa mafuta baharini.
- Utunzaji wa nyenzo/vifaa vya kukabiliana na kumwagika mafuta baharini / majini.
- Usafirishaji wa vifaa hadi bandari ya Tanga.
- Eneo la kazi la timu ya watoa huduma na wafanyakazi itakuwa ni Tanga (eneo la mradi).

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Makampuni yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi husika.
- Cheti cha Mlipa kodi cha Kampuni kwa mwaka uliopita 2022
- Leseni ya biashara inayothibitisha kufanya kazi hii kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili wa mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
- Orodha ya kina ya Nyenzo na Vifaa vya Kukabiliana na Kumwagika kwa Mafuta yenye uwezo wa kumudu umwagikaji wa mafuta baharini wa lita 10,000.
- Orodha ya wafanyakazi / Wataalamu wenye vyeti vyao vinavyotambulika kimataifa.
- Mpango mkakati au Muitikio wa Kuthibiti Kumwagika kwa Mafuta.
- Kuzingatia kanuni za petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu ,unapendekezwa sana.

Huu ni wito kwa kuonyesha maslahi au nia (EOI), umekusudiwa kutoa muongozo kwa watoa huduma kuonyesha uwezo na uzoefu kwa kutoa huduma za vifaa vya kuthibiti mafuta kumwagika baharini kwa namna itakayokidhi matarajio ya BBN Limited.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **9 Mei 2023, 12:00 jioni Saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

## HABARI KITAIFA

# Mwinyi aonya usafiri hatarishi, bandari bubu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi amewataka wananchi kuacha kutumia vyombo vya usafari wa baharini visivyozingatia usalama na kuepuka kutumia bandari bubu.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa boti mpya ya Kilimanyaro 8, Maruhubi mjini Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema kufanya hivyo kutahatarisha maisha yao na ni kinyume cha sheria.

Alisema, serikali yake itaendelea kuweka mazingira mazuri na kukaribisha wawekezaji kuleta vyombo vya usafiri baharini vyenye ubora na sifa za usalama. Pia alisema serikali itaendelea kufungua milango ya uwekezaji kwa kuweka mikakati bora ambayo itatoa nafasi kwa wawekezaji na sekta binafsi.

Dk Mwinyi alisema kampuni ya Azam imeonyesha mfano wa kampuni za kizalendo katika kuwekeza Zanzibar hatua ambayo imesaidia kukuza uchumi, pato la taifa na ajira.

Pia, alizitaka kampuni zingine kutumia fursa iliyopo ya serikali kufanya kazi na sekta binafsi katika kujenga uchumi wa Zanzibar, hivyo kuisaidia serikali katika usafiri wa majini nchini.

Rais Dk Mwinyi aliwasilisha ombi lake kwa kampuni ya Azam kuanzisha safari za boti za mwendo kasi katika kisiwa cha Pemba ili wananchi wafaidike na fursa hiyo ya huduma za haraka.

Alisema wananchi wanaokwenda Pemba wanachukua muda mrefu hadi kufika na wakati mwingine vyombo vya usafiri havifanyi safari kila siku.

"Nawasilisha ombi langu rasmin kwa kampuni ya Azam Marine kwa kuwa sasa zipo boti za kutosha. Kwa hiyo naomba muanzishe safari za mwendokasi katika kisiwa cha Pemba hadi Tanga kwa ajili ya kurahisisha usafiri," alisema.

Dk. Mwinyi pia alisema serikali inaendelea na mikakati yake ikiwamo ujenzi wa bandari shirikishi Mangapwani hatua ambayo itaongeza ufanisi na kupunguza msongamano katika bandari ya Malindi, mjini Unguja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bakhresa Group, Abubakar Said Bahressa, alisema wamefurahishwa na mazingira ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi ambayo inakwenda sambamba na sera ya uchumi wa bluu.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kufungua milango ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi hususan usafiri wa baharini ambayo kampuni hiyo imewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 120 na kutoa ajira kwa wananchi 400.

# Mwenyekiti CCM ajinyonga madai kudhulumiwa mil. 118/- za kahawa

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA



MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Mlowo, Mbozi mkoani Songwe, Meshack Mwambogolo, amekutwa amejinyonga msituni huku akiwa ameacha ujumbe wa kuitaka familia yake kumsamehe kutokana na uamuzi huo.

Mwili wa kiongozi huyo ulikutwa ukining'inia kwenye mti katika msitu ulioko kitongoji cha Iyenga, Kijiji cha Shaji Kata ya Mlangali wilayani humo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Theopista Mallya, aliwaambia wandishi wa habari jana kwamba mwili wa marehemu ulikutwa juzi asubuhi na kwamba alikutwa amejinyonga kwa kamba ya manila.

Alisema, uchunguzi wa awali uliofanywa na jeshi hilo ulibaini kuwa chanzo ni Mwambogolo kudhulumiwa fedha na rafiki yake ambazo zilikuwa kwa ajili ya ununuzi wa kahawa.

Alisema Mwambogolo alitoa Sh. milioni 118 na kuziweka kwenye akaunti ya rafiki yake, Joseph Muhume, kwa ajili ya kununulia kahawa lakini rafiki yake huyo alitokomea kusikojulikana na fedha hizo.

Kamanda Mallya alisema baada ya Mwambogolo kupewa taarifa kuwa Muhume ametoroka, alichukua kamba na chupa ya sumu ya kuulia wadudu ambayo hakuitaja jina na kutokomea navyo kabla ya mwili wake kukutwa ukining'inia kwenye mti.

"Alipopekuliwa mfukoni alikuwa na ujumbe ambao unasema: 'Naomba wana familia mnisamehe kwa uamuzi wangu wa kujinyonga.' Alikuwa ameandika kwa kifupi sana," alisema Mallya.

Aidha, Kamanda Mallya aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi ikiwamo kujiua na badala yake wafuate taratibu za kisheria kutatua matatizo yanayowakabili.

Katibu wa CCM Mkoa wa Songwe, Juma Mpeli, alikiri kupata taarifa hiyo na kwamba iliwasikitisha kutokana na uamuzi aliofanya kiongozi huyo kuwa mgumu.

Alisema, kutokana na tukio hilo kuwa na mazingira ya kutatanisha, waliamua kuliachia Jeshi la Polisi ili liendelee na taratibu za uchunguzi na hatua zingine za kichama zitafuata.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuwa watulivu wakati taratibu za vyombo vya ulinzi na usalama vikiendelea na uchunguzi.





**The United Republic of Tanzania**
**President's Office**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

## VACANCY ADVERTISEMENT

Tanzania Social Action Fund (TASAF) is currently implementing Productive Social Safety Net Program which aims at protecting the Vulnerable Poor Households from severest consequences of poverty by implementing interventions that will lead to increased household incomes and opportunities while increasing consumption.

The TASAF Executive Director is inviting applications from suitably qualified Tanzanian nationals to fill the below vacant posts:-

1. Director of Knowledge Management and Advocacy — 1 post
2. Communication Specialist — 1 post

Job Descriptions and required qualifications for these posts are available in TASAF website www.tasaf.go.tz

**How to apply**;

1) a) Applications, enclosing scanned certified copies of certificates and Curriculum Vitae be sent to the following address:-
**Executive Director**
**Tanzania Social Action Fund (TASAF) Kambarage Tower Building**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road**
**P.O. Box 2719**
**DODOMA.**
b) Applications (In PDF Format), enclosing scanned certified copies of certificates and Curriculum Vitae be sent through the following email address: **hr@tasaf.go.tz**
2) Applications made in a way other than the above will not be considered,
3) Deadline for receiving applications is **10th May, 2023.**

**Ladislaus J. Mwamanga**
**EXECUTIVE DIRECTOR**

217361201

# Uhai wa Hifadhi Saadani shakani

## ●Wanaopaswa kuilinda ndiyo wanaiangamiza

**Na Mwandishi Wetu**

UHAI wa Mbuga ya Wanyama Saadani uko shakani. Kile ambacho sheria zinazuia ili kulinda uasili wa mbuga, ndicho kinafanyika. Zile kanuni zinazolenga kukinga hifadhi, ndizo zinavunjwa. Mikono ya waliotarajiwa kutetea na kulinda urithi wa nchi na dunia, inaonekana kufaganzi.

Haya yanatokea wakati wasimamizi wa mbuga wakijipanga kuifanya Saadani kuwa Kitovu cha Utalii wa Ndani; wakianzisha utalii wa wikiendi (Ijumaa hadi Jumapili) kwa wakazi wa Dar es Salaam kwa safari za treni maalum huku wakipanga kuongeza safari za ndege na boti kwa watalii wanaopitia Zanzibar.

Watalii wanaoingia au kutoka nchini, kwa kupitia Zanzibar na Dar es Salaam, huenda wakashindwa kuepuka kishawishi cha kuwa na mapumziko ya siku mbili au tatu katika hifadhi ya Saadani kabla ya kuanza au kuendelea na safari zao kwingine.

Hayo yanaweza kutokea na kushamiri iwapo mbuga haitavurugwa kwa kuharibu ikolojia yake na kukatisha uhai wa mimea na wanyama ambavyo ni sehemu kubwa ya uasilli na utajiri wake.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, anashauri katika ripoti yake ya 2020/21, "...serikali ichukue hatua stahiki kunusuru mfumo wa ikolojia wa Hifadhi ya Saadani."

Kunusuru Saadani ni kuacha kutupa chochote mbugani ambacho hakikuwamo; kuondoa mifugo mbugani ili kuepusha mifugo kuambukizwa au kuambukiza magonjwa kwa wanyamapori, kupunguza au kuondoa kabisa kelele za binadamu na shughuli hasi kwa uasilia wa hifadhi; na kutoongeza au kupunguza mimea - miti hata maua ndani ya hifadhi.

Kifalsafa, hakuna uasili ulio nje ya utawala wa binadamu. Ataupenda uasili. Ataulea. Atautumia. Lakini atauharibu au kuuua. Hakuna mahali ambako binadamu hajaathiri - vizuri au vibaya - mipaka, maendeleo, uhai na uhalisia wa watu, vitu na uzuri wake.

Hata hivyo, hii siyo sababu ya kuharibu kila kitu hata chenye thamani na faida kwa watu na jamii. Hii ndio maana mbuga zinalindwa kisheria kwa manufaa ya jamii nzima ya dunia.

Hapa ndipo inaingia Saadani na mbuga nyingine. Adui wa uhalisia aliyebakia na asiyetawalika haraka, ni "mabadiliko ya tabianchi." Lakini naye, kwa sayansi iliyopo, aweza kutabiriwa, kuandaliwa mikakati na hatimaye kupunguza nguvu zake kwa uasili wa mtu na mazingira yake.

Hili pekee ndilo linahalalisha kuwapo sheria na kanuni za kulinda uasili wa hifadhi na familia za viumbe waliomo.

Kwa hiyo, kukata miti hifadhini, kujenga kiwanda hifadhini kwa ajili ya kuzalisha chumvi, kubakiza kijiji cha watu wapatao 1,500 ndani ya hifadhi, ambao wataongezeka na hatimaye kuhitaji shule, zahanati na huduma nyingine za msingi; ni kulea makusudi ya kuua mbuga na uasili wake.

Kukata mikoko ambayo inabugia hewaukaa kwa wingi kuliko mimea mingine, kunaacha jamii bila ulinzi. Kupiga kelele maeneo mbalimbali mbugani kunafukuza wanyama na kupunguza au kuondoa kabisa thamani ya hifadhi. Sheria ya Hifadhi za Taifa ya Mwaka 1959 inazuia yote hayo.

Ukiingiza mafuta na kemikali nyingine za mitambo, na vitu hivyo kumwagika au kumwagwa mbugani, mimea ambayo haihami, ama hukauka, huathirika vibaya au hufa, wataalamu wameonya.



Moja ya makazi yaliyokutwa katika Kitongoji cha Makupani karibu na mradi wa chumvi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mbuzi, mbwa na kuku wanaoranda misitu na mbuga ya Saadani, siyo wakazi halali na wa asili hifadhini. Hawa huweza kuangamizwa na wanyamapori, au hata kuchumbia wanyamapori kukaribia makazi ya binadamu na kuwadhuru au kuwaua.

Vilevile, mifugo mbugani kama ulivyo uchimbaji madini kwa maoni ya CAG ni shughuli ambazo "zinahatarisha mfumo wa ikolojia ndani ya hifadhi na hivyo kusababisha kutokuwapo uhakika wa uendelevu wa Hifadhi ya Saadani."

Saadani ina mto maarufu - Wami, wenye ikolojia inayohifadhi miti ya mikoko ambayo ni maarufu pia kwa kuhifadhi uoto wa asili wa misitu ya pwani na nyika, samaki, mamba, viboko na ndege wa majini.

Saadani pia ina misitu minene ya ukanda wa pwani (Zaraninge); ina makundi ya tembo, nyati, pundamilia, swala na simba; ina utalii wa fukwe na utalii wa boti ili kuona mamba na viboko.

Hata hivyo, yanayotendeka ndani ya Saadani yanakinzana na sheria za hifadhi nchini, na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), ambao pamoja na mambo mengine, unalenga kuimarisha vivutio vya utalii ili vichangie zaidi katika Pato la Taifa na kutoa fursa za ajira.

Kwa mujibu wa mpango huo, ifikapo mwaka 2026, idadi ya watalii nchini inatarajiwa kufikia milioni tano na mapato ya dola bilioni sita kwa mwaka, Hifadhi ya Taifa Saadani ikiwa sehemu ya mkakati huo wa kuwavutia wageni.

Mazingira ya sasa ya Saadani yanakinzana pia na Programu ya Utalii ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya 2020 - 2030 inayohimiza nchi wanachama wa jumuiya hiyo kuhakikisha kunakuwa na utalii endelevu na kuondosha vikwazo vya utalii na uhifadhi katika ukanda huo. Tanzania ni mwanachama mwasisi wa SADC.

Unahitaji kujua fikra na mipango ya sasa ya Saadani ili uelewe kuwa lolote la kukwaza hifadhi hiyo linaweza kuitwa hujuma ya makusudi.

Unahitaji kujua, kwa mfano, kuna matangazo yanakuja kwa wanaotaka kufanya uwekezaji chanya - hoteli na kumbi za starehe na mengine kwa watalii, ili kuinua ubora na umaarufu wa hifadhi.

Kwa mfano, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa hifadhi hiyo, Ephraim Mwangomo anasema kuna mpango wa kujenga gati la muda ili mbuga iwe inafikika kwa watalii wanaokuja kwa boti kutoka Dar es Salaam na Zanzibar.

Mwandishi ameoneshwa vifaa vya ujenzi. Kazi inapaswa kukamilika katika miezi mitatu ijayo; huku likisubiriwa gati la kudumu linalojengwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Tayari amepatikana mwekezaji kwa ajili ya usafiri wa boti, Aljazeera Marine Tours and Safaris ambaye shughuli zake za usafirishaji watalii zimepangwa kuanza Julai mwaka huu - akibeba watalii kutoka Zanzibar.

Utavutiwa na mpango kabambe wa kupeleka makundi ya watalii kwa ndege kutoka Zanzibar na Dar es Salaam hadi kiwanja cha ndege kilichoko ndani ya hifadhi "kwa bei chee" kama alivyoitaja Kamishna Mwangomo - dola za Marekani 1,200 kwa mtu mmoja au kundi la watalii watakaokuwa wanakwenda mbugani wakati huo. Anaitaja ni safari ya robo saa kutoka Zanzibar hadi hifadhini.

Lakini zogo linalotishia Hifadhi ya Saadani, halihusu mwekezaji na wakazi peke yake. Linahusu pia wanyama na wakazi wa mbugani kama ilivyo nchi nzima.

Katika ripoti yake, CAG Kichere anasema kulikuwa na visa 42 vya migogoro kati ya binadamu na wanyamapori kwenye hifadhi za taifa nchini vilivyosababisha vifo vya watu 26 na wengine 77 kujeruhiwa kwa mwaka 2021/22. Mwaka 2020/2021, kulikuwa na visa 31 vilivyosababisha vifo vya watu 20 na majeruhi 66.

CAG anataja sababu kuu ya vifo na majeruhi ni binadamu kuingilia hifadhi za wanyamapori, kama inavyoshuhudiwa Saadani kwa sasa.

Festo Ndahani (50), mkazi wa Kitongoji cha Makupani, ni shahidi wa zogo kati ya wanyamapori na binadamu. "Agosti 2021, nyati alinijeruhi kwenye mkono wa kulia na mguu wa kushoto," anaonesha.

"Kipindi hicho nilikuwa kibarua katika Kampuni ya Sea Salt Limited. Nyati alinikuta ninakata minyaa kwa ajili ya kupanda kwenye mabwawa ya chumvi. Kama si yowe niliyopiga wanakijiji wakaja kuniokoa, nisingekuwa hai," anaeleza.

"Nilikaa Muhimbili kwa wiki mbili. Matibabu yalikuwa Sh. 950,000. Wauguzi waliniambia 'nenda nyumbani, ukipata fedha, utalipa deni lako'," Ndahani anabainisha hajawahi kulipa. Hana kazi ya kumwingizia ujira.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Makupani, Mzee John Mbota (56), anasema changamoto kubwa zinazowakabili ni kuvamiwa na wanyamapori wakali hasa chui na nyati. Analitaja tukio la Aprili mwaka jana la kuvamiwa na nyati lililosababisha kifo cha mwanakijiji.

Mhifadhi Mkuu wa SANAPA, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Mwangomo, anathibitisha kuwapo uvamizi wa chui katika makazi ya wananchi na kuchukua mbuzi, hasa katika Kijiji cha Saadani.

Mwandishi aliamua kuingia hifadhini kujionea mwenyewe hali ilivyo. Kwa saa tatu alisubiri gari aina ya Noah kutoka Bagamoyo, lipate abiria 12 ili kwenda katika mradi wa chumvi. Ni kilometa 44 hadi Kijiji cha Gama kwa nauli ya Sh. 5,000. Baada ya hapo kuna safari ya kilometa 11 kwa pikipiki (bodaboda) kwa malipo ya Sh. 8,000 kukifikia Kitongoji cha Makupani.

Hii ni safari inayomwanzishia msafiri utalii kwa kuona aina mbalimbali za wanyamapori hifadhini kama vile tembo, simba, nyati na nyani ambao ndiyo wengi zaidi hifadhini (2,170). Msafiri anatalii mwanzo hadi mwisho bila kulipa chochote kwa mamlaka ya hifadhi - SANAPA.

Ndani ya Kitongoji cha Makupani, mna vibanda vilivyojengwa kwa miti na kukandikwa kwa udongo, huku vikiezekwa kwa makuti na vichache kwa mabati. Pia kuna nyumba nne zilizojengwa kwa matofali ya saruji na kuezekwa kwa mabati; na vibanda vingine viwili vilivyojengwa kwa mabati kuanzia chini hadi paa.

Pembeni kuna nyumba imara ambayo Mzee Mbota anasema ni kwa ajili ya viongozi wa kampuni hiyo; huku kukishuhudiwa mitambo ya uzalishaji chumvi, kuku wakiparua, na mbwa wakirandaranda katika kitongoji hicho.

Yalipo mabwawa (vyungu) ya kuvunia chumvi, pembeni (karibu na barabara) kuna mabango makubwa yenye maneno tisa (9) yaliyoandikwa kwa herufi kubwa kwa lugha za Kiingereza (juu) na Kiswahili (chini), yanayosomeka: PRIVATE PROPERTY, PHOTOGRAPH PROHIBITED (MALI BINAFSI, MARUFUKU KUPIGA PICHA).

Ni katazo ambalo Kamishna Mwangomo analilalamikia ni kinyume cha sera yao, kwamba picha ni sehemu ya utalii, picha ndiyo biashara ya utalii, ndiyo raha yenyewe ya utalii, hivyo mabango hayo yanasababisha mgongano wa chumvi na utalii.

Anarejea historia, kwamba wakati SANAPA inaanzishwa miaka 18 iliyopita, vijiji vya Saadani na Buyuni havikuondolewa mbugani, lakini "baadaye ikabainika Kitongoji cha Uvinje (kijijini Saadani) kinaingilia mno shughuli za hifadhi."

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu ya Mwaka 2012, Kijiji cha Saadani kilikuwa na wakazi 1,433 wakati Kijiji cha Buyuni kilikuwa nao 206.

Kamishna Mwangomo anasema tayari

**Inaendelea Ukurasa 5**

## Uhai wa Hifadhi Saadani shakani

Inatoka Uk.4

wakazi wa Kitongoji cha Uvinje wamefanyiwa taratibu za kulipwa fidia ili kupisha eneo la hifadhi, akifafanua, "...mwaka 2014, kaya 22 zilipwa fidia ya jumla ya Sh. 769,539,770 (milioni 769.54/-). Malipo ya ziada ya Sh. 287,631,000 (milioni 287.63/-) kwa wananchi 42 yanaandaliwa. Watalipwa katika mwaka ujao wa bajeti - 2023/24."

Kuhusu hoja ya ekari 728.17 kuendelezwa na Kampuni ya Sea Salt Limited bila kibali cha TANAPA, Kamishna Mwangomo anasema utatuzi wake uko chini ya Kamati Teule ya Mawaziri Wanane iliyofika Saadani Oktoba 2019, kushughulikia mgogoro huo unaoendelea.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Sea Salt Limited, Ajay Sengar, amemweleza mwandishi kuwa kuna mgogoro wa eneo kati yao na TANAPA; na kwamba wanasubiri utatuzi wake toka mamlaka za serikali.

Kwa mujibu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kampuni hiyo ilisajiliwa nchini mwaka 1998 ikiwa na mtaji wa Sh. bilioni 10 na shughuli zake kuu ni uchimbaji chumvi na madini mengine.

Kamishna wa Ardhi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Nathaniel Nhonge, amemwambia mwandishi kuwa mzozo huu "unashughulikiwa na Kamati ya Mawaziri Wanane" iliyoundwa na Rais John Magufuli mwaka 2019.

Kamishna wa Madini, Dk. Abdulrahman Mwanga, alimthibitishia mwandishi kuwa leseni Na. ML 05/92 ilitolewa kwa Kampuni ya Sea Salt Limited kwa mujibu wa sheria kwa kuwa mwekezaji huyo alifuata taratibu za kupewa leseni ya uchimbaji madini.

"Leseni inatolewa hata kama mwombaji hajafikia makubaliano na mwenye eneo kwa sababu kwenye madini kuna hatari aliyegundua madini akawahiwa.

"Sasa, ikishafikia hatua ya uchimbaji, lazima mwenye leseni ya uchimbaji amalizane na mwenye eneo.

Huwezi kuchimba bila kupata haki ya eneo husika, hapo mamlaka zingine za serikali zinaingia, kwa maana ya wizara yenye dhamana ya ardhi. Kama kuna tatizo kati yao na TANAPA, wanapaswa kulitatua kwa sababu huwezi kuendesha uchimbaji hadi ukubaliane na mwenye eneo," alifafanua.

Profesa wa Mifumo ya Ikolojia, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Idara ya Mifumo Ikolojia na Uhifadhi, Pantaleo Munishi amemwambia mwandishi kuwa takaoevu zitokanazo na uchimbaji madini ni hatari kwa afya ya viumbe hai na mazingira iwapo hazitadhibitiwa.

Prof. Munishi anafafanua, "Kwa hiyo, shughuli yoyote ya uchimbaji madini ndani ya hifadhi ina uwezekano wa kukimbiza ile baionuai, hasa wanyamapori kwa sababu ya kelele na usumbufu wa watu ambao wako pale kwenye mradi, wanyama watahama.

"Bahati mbaya taka kama hizi madhara yake huonekana baada ya muda mrefu. Mimi ninashauri uchimbaji madini kwenye maeneo ya hifadhi uachwe kwa sababu una athari kubwa katika mifumo ya kiikolojia kwa wanyama na mimea."

Bakari Mtiri, Mhadhiri Msaidizi wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Moshi, anashauri elimu itolewe kwa wananchi na wawekezaji ili kuwanusuru wanyamapori.

Ofisa Miradi wa Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifwani, anashauri Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) litumie mamlaka yake chini ya kifungu cha 99(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004, kufika eneo la uzalishaji chumvi kule Saadani na kufuatilia ni kwa kiasi gani shughuli hizo zinaathiri mazingira na mfumo wa ikolojia wa hifadhi.

"Iwapo ufuatiliaji utaonesha mzalishaji wa chumvi alikiuka sheria kwa kutofuata masharti ya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA), NEMC watapaswa kutumia mamlaka waliyonayo chini ya kifungu cha 100(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kumtaka mzalishaji chumvi kusafisha mazingira, pia kuchukua hatua zitakazoelekezwa ili kuyarudisha mazingira katika ubora wake wa awali," anasema.

"NEMC wana dhamana kubwa ya ulinzi wa mazingira. Wakitekeleza wajibu wao kikamilifu, watalinda hifadhi za taifa, wataongeza mapato ya serikali na zaidi ya yote, watawalinda wanyamapori na kuwahakikishia kuishi katika mazingira safi na salama," anashauri.

Kamishna Mwangomo anasema SANAPA ambayo ni Hifadhi ya Taifa ya 13 kuanzishwa nchini kati ya 22 zilizopo chini ya TANAPA, sasa ina waajiriwa 83; kati ya hao, 18 ni wanawake; na asilimia 60 ya waajiriwa wote ni askari-pori.

# Wadau wa habari watinga Dodoma kuteta na wabunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TIMU ya Wadau wa Haki ya Kupata Habari (CoRI), imetua jijini Dodoma kwa lengo la kukutana na wabunge ili kufafanua zaidi mapendekezo ya mabadiliko ya vipengele vya sheria viliyoachwa nje kwenye muswada wa sheria ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016 uliowasilishwa bungeni Februari 10 mwaka huu.

Wajumbe hao wa CoRI ni pamoja na Deus Kibamba; Saumu Mwalimu, Baraza la Habari Tanzania (MCT); Neville Meena, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) na James Marenga, Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN).

Deus Kibamba, Mjumbe wa CoRI alisema jana kuwa lengo ni kuhakikisha wabunge wanaelewa zaidi dhamira ya waandishi wa habari na uhuru wa habari nchini.

"Bado tuna imani wabunge watatuelewa, tumekuja kukutana nao ili tueleze zaidi kwa nini baadhi ya vifungu vilivyoachwa nje ni muhimu kuingia kwenye muswada," alisema.

James Marenga kutoka MISA TAN alisema wabunge ndio watunga sheria na muswada umeishafikishwa kwao, hivyo ni muhimu kukutana nao.

"Tulianza na serikali na wakatusikiliza, wakawasilisha kile walichowasilisha bungeni. Ni wakati sasa na sisi kukutana na wabunge kwa ufafanuzi zaidi, ninaamini wabunge ni waelewa na watatuelewa," alisema Marenga ambaye ni wakili wa kujitegemea.

Neville Meena kutoka TEF, alisema kinachofanywa na CoRI (kukutana na wabunge) ni jambo la kawaida pale kunapokuwa na hatua za utungwaji wa sheria.

"Tumeona ni fursa kwetu sasa kukutana na wabunge ili kuwaeleza nini tunapigania na kwanini. Nafasi hii tunapaswa kuitumia vizuri na ndio maana tupo hapa Dodoma," alisema.

Akizungumza kwenye mkutano wa wadau hao uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 20 Februari 2023, Deodatus Balile, Mwenyekiti wa TEF, alisema ni muhimu kwa CoRI kukutana na wabunge ili kushawishi baadhi ya vipengele 'vilivyotelekezwa' kwenye muswada huo.

"Tutakwenda kuzungumza na wabunge kuhusu athari zinazoweza kuifika tasnia ya habari kutokana na baadhi ya vifungu vilivyomo kwenye sheria na marekebisho yaliyofanywa na serikali ili watusaidie kurekebisha siku wakianza kujadili bungeni," alisema.

Miongoni mwa vipengele ambavyo CoRI wanataka viingizwe kwenye muswada wa sheria kabla ya kujadiliwa ni sehemu ya saba inayohusu adhabu na makosa yake, wakipendekeza kupungua adhabu hasa kwa makosa yanayohusu taalamu.

Walipendekeza serikali iondoe ukomo wa chini wa adhabu kwa vifungu vyote kwa kuwa inambana hakimu au jaji kuamua vinginevyo.

Pia wanasema kifungu cha 7(2) kinaeleza kuwa serikali inaweza kutoa agizo habari fulani kuchapisha au kutangaza habari kwa kuwa ina umuhimu kwa Taifa

CoRI wanasema kifungu hicho ni kuingilia uhuru wa uhariri kwa kuwa uhariri unafanywa nje ya chumba cha habari ambacho kina watu wenye weledi na uzoefu mkubwa.

CoRI wanalalamikia kifungu cha 5(e)a,b kinachohusu utoaji wa leseni ambapo Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), anaweza kukataa maombi ya leseni au kuhuisha kulingana na matakwa yake.

Wanasema kifungu hicho pia kinampa mamlaka ya kusitisha leseni wakati wowote anapoona chombo husika hakina mwenendo anaoutaka yeye.

# Mahakama yatupa rufani aliyembaka mwanafunzi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu imetupilia mbali rufani iliyowasilishwa na Harison Kaale akipinga kifungo cha miaka 30 jela alichohukumiwa kwa kosa la kubaka mwanafunzi baada ya kuona haina mashiko, hivyo kubaki aendelee kutumikia adhabu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Mahakama Kuu Kanda ya Moshi mbele ya Jaji Safina Simfukwe, baada ya kupitia sababu tatu za rufani na majibu ya upande wa Jamhuri.

Mrufani alishtakiwa katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi kwa kosa la kubaka na alitiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Ilidaiwa Aprili 15, 2021 maeneo ya Mwika Karueni mkoani Kilimanjaro, mrufani alimbaka mwanafunzi wa miaka 15 na aliposomewa shtaka alikana.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, binti alikuwa akienda shuleni nyuma kulikuwa na mrufani na alipomfikia alimsalimia lakini hakuitika badala yake alimwinua akamweka shingoni kisha akampeleka kwenye shamba.

Alipomfikisha shambani, ilidaiwa alimvua sketi na nguo zake za ndani na kumziba kisha mdomo akambaka, akatoweka na kumwacha binti akiwa anatokwa damu mdomoni na sehemu za siri.

Ilidaiwa kuwa baada ya mrufani kuondoka, binti alipata nafasi ya kupiga kelele kuomba msaada na mwanafunzi mwingine ambaye ni shahidi wa tatu, alisikia kilio akasogea eneo la tukio na kumkuta mwenzake akilia na alipomwuliza, alidai kuwa alibakwa.

Wakiwa katika eneo hilo wakiomba msaada, alifika shahidi wa pili, akamchukua binti na kumpeleka kwa wazazi wake ambao walikwenda Polisi wakapewa PF3 kisha akapelekwa hospitalini kwa ajili ya matibabu na uchunguzi.

Mrufani alikana kuhusika na tukio hilo akidai kwamba mashtaka yake ya kupandikizwa kwa sababu ametofautiana na baba wa binti huyo.

Akipinga adhabu ya kifungo, alitoa sababu tatu, akidai mahakama ilikosea kusema kuwa mashtaka dhidi yake yalithibitika bila kuacha shaka. Pia alidai kuwa mahakama ilikosea kusema kwamba PF3 iliyotolewa kama kielelezo inatosha kumtia hatiani mrufani.

Katika sababu ya mwisho, alidai Mahakama ilikosea kusema kwamba umri wa binti ulithibitishwa mahakamani.

Wakili wa Mrufani, Gideon Mushi, alidai mashtaka dhidi ya mrufani hayakuthibitishwa bila kuacha shaka dhidi ya mteja wake, hivyo aliomba mahakama ikubali rufani, imfutia hatia, adhabu na imwachie huru mteja wake.

Wakili wa Serikali, Grace Kabu, alijibu akidai kuwa mashtaka dhidi ya mrufani yalithibitishwa bila kuacha shaka. Alidai sababu za mrufani hazina mashiko, hivyo aliomba mahakama ibariki hatia na adhabu dhidi ya mrufani viendelee.

Jaji Simfukwe baada ya kusikiliza rufani hiyo, alisema mahakama inaona upande wa Jamhuri ulithibitisha mashtaka dhidiyamrufanibilakuachashaka, hivyo kubariki adhabu hiyo iendelee.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Wananchi wachukue hadhari matumizi ya vinywaji 'energy'*

**VINYWAJI** vya kuongeza nguvu, maarufu kama 'enegy', vimekuwa vikishabikiwa sana na watu wa marika mbalimbali nchini na kuvitumia kama sehemu ya kuondoa uchovu mwilini au kuchanganya na vinywaji vikali kwa kile kinachodaiwa ni kupunguza mning'inio na kutopata usingizi.

Kwa kupanda chati huko, kampuni mbalimbali nchini zimekuwa zikitengeneza bidhaa hiyo kutokana na kupendwa huku vingine vikiagizwa kutoka nje. Watumiaji wakubwa wa vinywaji hivyo ni madereva wakiwamo wa mabasi ya abiria ndani ya miji, maarufu kama daladala na wale wa mabasi na magari makubwa ya safari ndefu kwa kile kinachoelezwa kuwa kinawafanya wasichoke wakiwa kazini.

Watumiaji wengine wa kiwango cha juu cha 'energy' ni wanamichezo kwa kuamini kuwa wanapofanya hivyo wana uwezo wa kupata nguvu wakati wa mchezo. Kutokana na kuchangamkiwa na watu kwa kiasi kikubwa, hivi sasa katika maduka makubwa, madogo na sehemu za starehe kama hoteli na baa, vinywaji hivyo vinapatikana kwa wingi na vinanunuliwa kwa kasi.

Tayari serikali imeshaonya juu ya matumizi ya vinjwaji hivyo kutokana na kuwa na madhara makubwa ya afya. Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imeshaonya matumizi hayo kutokana na kupokea wagonjwa wengi wenye maradhi ya moyo ambayo historia yao inahusishwa na matumizi ya 'enegy'. Kwa mujibu wa taasisi hiyo, wagonjwa wengi wamekuwa wakifika kwa matibabu, wengi wakiwa na historia zinazofanana za matumizi ya vinywaji hivyo.

Wataalamu wa JKCI wamebainisha kwamba matumizi ya 'energy' yana athari kubwa kiafya kwa kuwa mtu anapotumia, baada ya dakika kadhaa caffeine huingia kwenye mzunguko wa damu hivyo kusababisha mtu kupatwa na shinikizo la damu na mapigo ya moyo kuwa katika hali isiyokuwa ya kawaida.


Hivi karibuni, mathalan, katika taasisi hiyo ilielezwa kuwa kijana wa miaka 21 alifikishwa hospitali akiwa na hali mbaya na baada ya uchunguzi, ilibainika kuwa alizidisha matumizi ya kinywaji hicho. Kwa mujibu wa taarifa hiyo kijana huyo alikuwa na maumivu makali ya kifua upande wa kushoto ulipo moyo na uchunguzi ulibaini kwamba alipatwa na matizo hayo kutokana na utumiaji wa vinywaji vya kuongeza nguvu na kuwa kwa siku sita alikuwa amekunywa makopo matano kila moja likiwa na ujazo wa milimita 250.

Kama vile haitoshi, kijana huyo inasemekana alikuwa amekunywa lita moja na robo ya kinywaji hicho ndani ya saa nne na baada ya kumaliza kopo la mwisho, ndipo alipopatwa na mkasa huo na hatimaye kwenda hospitalini. Matumizi hayo ya kinywaji yalisababisha mishipa ya moyo kuziba, upande wa kushoto ukiziba kwa asilimia 100 na kama hali hiyo ingeendelea kwa saa kadhaa, misuli ya moyo ingekufa na hatimaye kukumbwa na kifo cha ghafla.

Kuwapo kwa taarifa hiyo, kumesababisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuiagiza Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kufanya uchunguzi zaidi kuhusu matumizi ya vinywaji hivyo ili kupata ushahidi wa kisayansi.

Pamoja na serikali kuagiza uchunguzi kufanyika, ni vyema wanaotumia vinywaji hivyo, wakiwamo vijana na makundi yaliyotajwa, kuchukua tahadhari ili kuepukana na madhara yanayoweza kuwapata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Manufaa kwa umma kupitia Jamii Forum inayomulika utawala bora*

Na Beatrice Moses

**TAASISI** ya JamiiForums (JF), kupitia mpango mkakati wake wa miaka mitano kati ya 2020 na 2024, imeamua kuwashindanisha wananchi katika kuongeza ubora wa maudhui ya lugha ya Kiswahili mtandaoni, yanayolenga kuchochea mabadiliko chanya na kufanya uwapo wa uwajibikaji na utawala bora nchini.

Shindano linajulikana 'Stories of Change' linakuwa ni shindano la tatu kufanywa na asasi hiyo, ambayo imetenga shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuwapatia zawadi watu watano watakaoshinda kwa kuandika machapisho yao yatakayotolewa kupitia kwenye mtandao wao wa JamiiForum.

JamiiForums (JF) ni asasi ya kiraia inayufanya uchechemuzi wa haki za kidigitali, demokrasia, uwajibikaji na utawala bora nchini. Vilevile, JF inaratibu jukwaa la tovuti JamiiForums.com, ambalo linatajwa kuwa tovuti namba moja nchini yenye rekodi ya kufikia watu zaidi ya milioni 3 kila siku.

Awamu ya kwanza ya shindano hilo ilifanyika kuanzia Julai hadi Oktoba 2021, ambayo jumla ya wananchi 1,509 walishiriki na kuandika jumla ya machapisho 1,536, huku 936 yakipitishwa kuingia kwenye shindano. Washindi watano wa kwanza walikabidhiwa zawadi mbalimbali katika hafla iliyofanyika, mjini Dar es Salaam mwezi, Oktoba 2021.

Awamu ya pili ya shindano, ikafanyika kuanzia Julai mpaka Septemba 2022 ambayo wananchi 1,820 walishiriki na kuandika jumla ya machapisho 2,073 huku 1,462 yakipitishwa kuingia kwenye shindano. Washindi bora kumi walikabidhiwa zawadi mbalimbali katika hafla iliyofanyika Dar es Salaam, mnamo Novemba 2022.

Katika maelezo yake aliyoyatoa kwa waandishi wa habari kuhusu shindano hilo, Mkurungezi wa JF, Maxence Melo, akabainisha kuwa miongoni mwa maudhui yaliyowasilishwa kwenye mashindano ya awali, yamechangia kufanyika maboresho katika mifumo ya utoaji huduma serikalini, huku baadhi ya taasisi zikipokea mapendekezo na kuahidi kuyafanyia kazi.

Ni hatua njema inayotajwa kutoa nafasi kwa wananchi kuwasilisha hoja ama dukuduku zao kwa namna inayobainisha mahali ambako kuna viongozi, lakini wameshindwa kuwajibika kwenye majukumu yao, hivyo kusababisha kero ya kukosekana huduma zilizokusudiwa.

Naamini zawadi iliyowekwa itakuwa ni kichocheo kizuri cha kuwezesha kuibuliwa kwa mengi ambayo, pengine yalikuwa yanafumbiwa macho kwa namna fulani.

Hivi karibuni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alitoa ripoti yake ya mwaka 2021/22 na taarifa ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ambayo ilibainisha mambo mengi yanayoonyesha kuna tatizo kwenye uwajibikaji.

Miongoni mwa yaliyobainishwa, ni pamoja na kuwapo gharama ambazo serikali inaingia kutokana na ucheleweshaji malipo au mikataba ambayo kwa hakika yanachelewesha maendeleo ya nchi na kusababisha mambo kuwa magumu kwa wananchi, hasa wanopata kipato cha chini na kati .

Kwenye kitabu cha Mwongozo wa Utawala Bora cha mwaka 2013, ambacho ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini, pamoja na jukwa la kisera maarufu 'Policy Forum' ya kukuza utawala bora nchini, kuna mambo kadhaa kimebainisha ikiwamo kueleza maana ya utawala .

Kwamba utawala ni matumizi ya mamlaka ya kisiasa, kiuchumi au vinginevyo katika kusimamia masuala ya nchi kwenye ngazi zote. Pia, utawala bora ni matumizi ya mamlaka yanapokuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu usawa na unafuata utawala wa sheria.

Ili kutekeleza dhana ya utawala bora, kunatajwa mambo yafuatayo lazima yazingatiwe: Matumizi sahihi ya dola; matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi; matumizi mazuri ya madaraka yao; kujua na kutambua madaraka waliyo nayo; na matumizi yake; pia madaraka yanayotumika kulingana na mipaka iliyowekwa .

Faida za Utawala Bora hadi sasa zinabainishwa kuwa ni unasaidia kuwa na mambo yafuatayo: Matumizi mazuri ya rasilimali za nchi; maendeleo endelevu; kupungua kwa umasikini; ujinga na maradhi; kutokomea kwa rushwa; huduma bora za jamii amani na utulivu; kuheshimiwa haki za binadamu; utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa sheria na taratibu; na kuleta ustawi wa wananchi.

## Brela yataka pingamizi Chalinze Cement kusubiri uamuzi wa FCT

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesema pingamizi lililowekwa na Kampuni ya Saruji ya Chalize katika Baraza la Ushindani wa Kibiashara (FCT) kuizuia kampuni ya Saruji ya Twiga kununua hisa za kampuni ya Tanga Cement kusubiri uamuzi wa baraza hilo

Majibu hayo yamekuja baada ya kampuni ya Twiga kuiandikia barua ya kutaka kujua kama kampuni ya Chalize imesajiliwa na kama ina nguvu ya kisheria ya kupinga uamuzi wake wa kutaka kununua hisa hizo.

Hivi karibuni kuliibuka mjadala juu ya mpango wa kampuni ya Saruji ya Twiga, kutaka kununua zaidi ya asilimia 60 ya hisa za Tanga Cement, hivyo kusababisha baadhi ya wadau wakiwamo Chama cha Watumiaji wa Saruji na Chalinze Cement kupinga uamuzi huo FCT kwa madai kuwa itasababisha bei ya bidhaa hiyo kupanda na kuwapo kwa ukiritimba katika soko.

Majibu kutoka BRELA yalithibitisha kuwa waliifutia usajili kampuni ya saruji ya Chalize tangu mwaka 2019 kwa mujibu wa kifungu cha 400 A cha Sheria ya Kampuni Sura ya 212 baada ya kukosa vigezo.

Taarifa iliyotolewa na Aprili 21 na Msajili wa Kampuni wa BRELA, Meinrald Mwenyemamu, imeonyesha kuwa kampuni hiyo ilifutwa usajili wake kwenye daftari baada ya kugundulika kuwa ilitoa taarifa za uongo wakati wa usajili ikiwamo kuwasilisha anwani ya kampuni ambayo haipo.

Aidha, taarifa hiyo ilibainisha kuwa kampuni hiyo haikuwa na uwezo wa kuzalisha saluji kwa kuwa mpaka inafungiwa haikuwa na leseni ya Daraja A inayoiwezesha kuzalisha bidhaa hiyo.

Kuhusu pingamizi lililowekwa na kampuni hiyo FCT kama lina nguvu kisheria, taarifa hiyo ilieleza kuwa ni vyema mlalamikaji akasubiri uamuzi wa baraza kwa kuwa suala hilo liko katika chombo hicho.



Mganga mkuu wa serikali Prof. Tumaini Nagu (Kulia) akimpa chanjo mtoto jana kwenye uwanja wa Kwaraa uliopo Mjini Babati ikiwa ni uzinduzi wa chanjo ya Surua Rubella kitaifa uliofanyika mkoani Manyara na alimwakilisha waziri wa Afya Ummy Mwalimu.**PICHA: JALIWASON JASSON**

# Serikali kutekeleza mkakati kukuza ujuzi, stadi kazi vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeliambia Bunge namna inavyotekeleza mkakati wa kukuza ujuzi na stadi kwa vijana unaolenga kuhakikisha nguvu kazi ya vijana inashiriki kwenye kujenga uchumi wa Taifa ambao hadi sasa wamenufaika 118,415.

Aidha, mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa unalenga kuwafikia vijana 681,000 na tayari serikali imeanza makubaliano na wadau wa maendeleo ili kuhakikisha mafunzo ya ujuzi na stadi yanatolewa kwa vijana na kuwatafutia ajira ndani na nje ya nchi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, VIjana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliyasema hayo jana bungeni alipookuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Latifa Khamis Juakali.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kukuza ujuzi na stadi kwa vijana.

Katambi alijibu ili kukuza ujuzi na stadi za kazi kwa vijana, serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ujuzi wa Miaka 10 (2016/17 - 2025/26) ambao umelenga kuhakikisha nguvu kazi ya vijana kushiriki katika kujenga uchumi wa taifa.

Alibainisha kuwa mkakati huo unatekelezwa kupitia programu na mipango mbalimbali ya kukuza ujuzi na stadi kwa vijana inayotekelezwa na wadau mbalimbali wakiwwmo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

"Baadhi ya programu na mipango hiyo ni pamoja Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambayo tangu kuanza kutekelezwa mwaka 2016/17 imetoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa jumla ya vijana 118,415 na Mpango wa Mafunzo na Uwezeshaji wa Vijana kushiriki kilimo unaotekelezwa na Wizara ya Kilimo unaojulikana kwa jina la Building Better Tomorrow (BBT)," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamani, alihoji serikali inatumia mfumo gani kutathmini tija na utekelezaji wa programu hizo hasa ikizingatiwa kasi kubwa ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia iliyopo sasa.

"Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vijana wengi wananufaika na program hizi hasa ikizingatiwa uhitaji ni mkubwa kuliko nafasi zinazopatikana,"alisema.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Katambi alisema chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuna timu ambayo hufanya tathmini pamoja na kuweka kanzidata.

"Moja ya mikakati ambayo serikali imeweka kuhakikisha vijana wengi wananufaika ni pamoja na huo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa kuhakikisha wengi wanaingia kwenye uchumi wa bluu ni pamoja na ufugaji wa Samaki lakini mkakati mwingine ni wa ukuzaji ujuzi ambao tumefundisha vijana 74,598, mwingine ni mkakati ambao upo chini ya Wizara ya Kilimo ambao tayari vijana 821 wamechukuliwa," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa 31.03.2023 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31.12.2022 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 53,016 | 54,749 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 81,056 | 60,422 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 124,814 | 103,603 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 59,605 | 69,156 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 248 | 271 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 141,652 | 98,960 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 858,295 | 841,590 |
| | 12 | Mali Nyingine | 43,222 | 39,970 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 20,511 | 21,207 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,382,419** | **1,289,929** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 919,076 | 862,393 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 113,407 | 124,778 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 2,537 | 2,206 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | (0) | (0) |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 21,369 | 24,428 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 2,641 | 2,641 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 29,473 | 28,084 |
| | 28 | Madeni | 145,959 | 129,401 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,234,461** | **1,173,931** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **147,958** | **115,998** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 31,372 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 73,656 | 71,781 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,393 | 3,152 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 40,537 | 9,694 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **147,958** | **115,998** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 157,474 | 151,019 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 78,024 | 72,800 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,703 | 15,323 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 2,396 | 1,736 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.70% | 8.99% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.83% | 8.43% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 85.56% | 87.44% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 62.09% | 65.24% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.36% | 80.95% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 4.59% | 0.50% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 7.17% | -0.08% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-22 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 34,839 | 34,722 | 34,839 | 34,722 |
| 2 Gharama za Riba | (12,858) | (10,604) | (12,858) | (10,604) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **21,981** | **24,119** | **21,981** | **24,119** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (10) | (16) | (10) | (16) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,406) | (3,481) | (2,406) | (3,481) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **8,868** | **7,904** | **8,868** | **7,904** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 1,641 | 1,422 | 1,641 | 1,422 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 5,210 | 4,139 | 5,210 | 4,139 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 2,017 | 2,342 | 2,017 | 2,342 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(24,755)** | **(24,673)** | **(24,755)** | **(24,673)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 12,854 | 12,346 | 12,854 | 12,346 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1,732 | 1,554 | 1,732 | 1,554 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 10,169 | 10,773 | 10,169 | 10,773 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,677** | **3,853** | **3,677** | **3,853** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,285 | 1,973 | 1,285 | 1,973 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,393** | **1,880** | **2,393** | **1,880** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **2,393** | **1,880** | **2,393** | **1,880** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,073 | 1,089 | 1,073 | 1,089 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 76 | 67 | 76 | 67 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 52 | 47 | 52 | 47 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.17% | 0.16% | 0.17% | 0.16% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.88% | 1.63% | 1.88% | 1.63% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.64% | 57.88% | 56.64% | 57.88% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.99% | 2.46% | 1.99% | 2.46% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-23 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-22 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 3.677 | 549 | 3.677 | 3.853 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 4.977 | 6.371 | 4.977 | 5.939 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (16.704) | (19.712) | (16.704) | (14.394) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 45.312 | 4.868 | 45.312 | 29.996 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (3.029) | (181) | (3.029) | (2.611) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (3.251) | 3.933 | (3.251) | (4.133) |
| - Kodi Iliyolipwa | (1.285) | (3.074) | (1.285) | (1.973) |
| - Mengineyo (bainisha) | (22.359) | (3) | (22.359) | 19.362 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **7,338** | **(7,249)** | **7,338** | **36,040** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (611) | (728) | (611) | (980) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | - |
| Mengineyo (fedha iliyotolewa na serikali) | 30.000 | - | 30.000 | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **29,389** | **(728)** | **29,389** | **(980)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (1,395) | (1,652) | (1,395) | (1,798) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(1,395)*** | ***(1,652)*** | ***(1,395)*** | ***(1,798)*** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 35,332 | (9,629) | 35,332 | 33,261 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **87,795** | **97,424** | 87,795 | **111,676** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 123,127 | 87,795 | 123,127 | 144,937 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziad ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **31,372** | - | **74,932** | **(0)** | **0** | **9,694** | **115,998** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 2,393 | **2,393** |
| Mapato mengineyo | - | - | (431) | - | - | (3) | **(434)** |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | | | (844) | 844 | | | |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo(Fedha iliyotolewa na serikali) | - | - | - | - | | 30,000 | **30,000** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **73,658** | **844** | **0** | **42,084** | **147,958** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 3,152 | - | - | - | **3,152** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hisa za ziada(Issued bonus shares) | **3,667** | - | **(3,667)** | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo(Kodi ya Hisa za ziada-W/t on bonus share) | **(367)** | | | | | - | **(367)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **74,932** | **(0)** | **0** | **9,694** | **115,998** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI, 2023

Benki ililipa faini ya shilingi 140,000/=kutokana na upungufu wa fedha zilizopelekwa Benki kuu(Bot counter shortage) Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| SABASABA K. MOSHINGI **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | Imesainiwa | 20.04.2023 |
| REGINA E. SEMAKAFU **(Mkuu wa Fedha)** | Imesainiwa | 20.04.2023 |
| SOSTHENES F. NYENYEMBE **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | Imesainiwa | 20.04.2023 |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| DR. EDMUND B. MNDOLWA **Mwenyekiti wa Bodi** | Imesainiwa | 20.04.2023 |
| MS. ANNE C. MBUGHUNI **Mjumbe wa Bodi** | Imesainiwa | 20.04.2023 |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

217389702

## TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES 2023

*All charges are VAT exclusive.

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | MINIMUM OPERATING BALANCE | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | 7,000.00 | 5.00 | 50,000.00 | 100.00 |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | FREE | N/A | 50,000.00 | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | 1,800.00 | 0.86 | 20,000.00 | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | 1,800.00 | N/A | 0 | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000.00 | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | FREE | FREE | 50,000.00 | N/A |
| Platinum Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 5,000 | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | FREE | N/A | 20,000 | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 0 | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000 | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | FREE | N/A | 30,000 | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | 1,800.00 | N/A | 10,000 | N/A |
| Wadu Account | FREE | N/A | FREE | FREE | 10,000 | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | 700.00 | N/A | 1,500.00 | N/A |

### CASH SERVICES

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Cash deposit | | FREE |
| | Withdrawal below 400,000 | 1,800.00 |
| | Withdrawal 400,001 - 800,000 | 3,000.00 |
| | Withdrawal from 800,001 - 1,200,000 | 4,400.00 |
| | Withdrawal from 1,200,001 - 10,000,000 | 5,000.00 |
| | Withdrawal from 10,000,001 - 50,000,000 | 6,000.00 |
| | Withdrawal from 50,000,001 -100,000,000 | 14,000.00 |
| Cash withdrawal TZS | Withdrawal from above 100,000,000 | 0.12% max 170,000 |
| | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| **BANK STATEMENT** | **TZS** | **USD** |
| Balance enquiry over the counter | 1000.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| **CHEQUE SERVICE** | **TZS** | **USD** |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00 per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

### AGENT BANKING SERVICE

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 3,000, 000.00 | 10,000.00 |
| Balance Enquiry | | 300.00 |
| Mini Bank Statement | | 300.00 |

### POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Registration | | FREE |
| | 500 -10,000.00 | 850.00 |
| | 10,000.01 - 50,000.00 | 1,200.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 1,500.00 |
| | 100,000.01 - 250,000.00 | 2,800.00 |
| | 250,000.01 - 500,000.00 | 4,600.00 |
| | 500,000.01 - 750,000.00 | 7,500.00 |
| Transfer Bank to MNO | 750,000.01 - 1,000,000.00 | 10,000.00 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

### LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

| LOANS | CATEGORY | RATE |
|---|---|---|
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 20,000.00 |
| | Loan Application fee | TZS 20,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 20,000.00 Maximum TZS 150,000.00 |
| | MIC loan Application fee | TZS 150,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 150,000.00 |
| | Loan Application fee for Business Loans | TZS 20 0,000.00 |
| Charges on Business Loan | Loan Administration fee - Business and Personal loans | 2% of the Approved Amount |

| DORMANT ACCOUNT | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

### POPOTE ATM SERVICE

| ACTIVITY | BAND[TZS] | New Charge (TZS) |
|---|---|---|
| 1. ATM Cash Withdraw | 1,000 – 99,000 | 1,500 |
| | 100,000 – 400,000 | 1,700 |
| 2. Interbank transfer on ATM | 1 – 99,999 | 1,300 |
| | 100,000 - 199,999 | 1,700 |
| | 200,000 - 299,999 | 1,700 |
| | 300,000 - 399,999 | 1,700 |
| | 400,000 - 499,999 | 2,500 |
| | 500,000 - 599,999 | 3,000 |
| | 600,000 - 699,999 | 3,500 |
| | 700,000 - 999,999 | 4,000 |
| | 1,000,000 - 1,999,999 | 5,000 |
| | 2,000,000 - 2,999,999 | 6,000 |
| | 3,000,000 - 3,999,999 | 7,000 |
| | 4,000,000 - 4,000,000 | 8,000 |
| 3. Intra-Bank Transfer on ATM | Any Amount | 1,000 |
| 4. Balance Inquiry | NA | 400 |
| 5. Mini Statement | NA | 400 |
| 6. Popote ATM card issuance /Replacement | N/A | 15,000 |
| 7. PIN Re-issue | N/A | 1,000 |
| 8. Collection of ATM card at non-domicileBranch | N/A | 6,500 |
| 9. Uncollected and Destroyed ATM Card | N/A | |
| 10. Card Maintainance | N/A | 5,000 |
| 11. Failed Transaction Due to insufficient fund | | 900 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

### GUARANTEE

| | CHARGES |
|---|---|
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

### POPOTE VISA CARD


| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote VISA issuance/Replacement | 20,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,350.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 5,500.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |




217389702

Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683 Namba bila Malipo: 0800110160



# Mkwawa yawakumbuka watoto yatima

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMPUNI ya ununuzi wa tumbaku ya Mkwawa iliyoko Kahama mkoani Shinyanga, imewakumbuka watoto yatima kutoka katika vituo vitatu kwa kutoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 13 kama sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii hasa wa makundi maalumu baada ya kununua na kuuza zao hilo.

Vituo hivyo ni pamoja na Jumuia ya Zawiyatul Qadriya ya Kahama, Muvuma na kituo cha Amani. Vitu vilivyotolewa ni pamoja na sabuni, sukari, mashuka, mchele, magodoro, mafuta ya kupikia na vyandarua kwa ajili ya kujikinga na malaria.

Akikabidhii msaada huo juzi, Meneja wa Kampuni hiyo, Alawi Sharrif, alisema fedha zilizotumika kununulia vitu hivyo ni sehemu ya faida wanayoipata baada ya kununua na kuuza tumbaku, hivyo wanarejesha fadhila kwa wananchi husussani makundi yenye uhitaji.

Yatima na wajane, alisema wana mahitaji kama walivyo watu wengine, hivyo ni wajibu wa kila aliye na kidogo kutoa kugawana nao ili wamudu maisha yao ya kila siku hususani katika vituo wanapokewa huku akiwasihi kutumia vitu hivyo kwa matumizi sahihi na si kuuzwa.

"Vitu hivi vina thamani ya Sh. milioni 13 na fedha hizo ni sehemu ya faida tunayoipata baada ya kununua na kuuza tumbaku yetu. Tunawasihi wengine nao kujenge tabia ya kutembelea makundi ya namna hii na kuyasaidia kwa sababu nao wana mahitaji," alisema Sharrif.

Mlezi wa Jumuiya ya Zawiyatul Qadriya, Hamad Hillal, alisema kituo kina watoto 35 na msaada umewafikia katika muda mwafaka na atahakikisha kila mtoto ananufaika nao. Aliwaomba wengine kujitokeza na kuwasaidia katika malezi kwa kutoa mahitaji.

Katika hatua nyingine, mjumbe kutoka Baraza la Wakurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Tanzania, Saidi Shabani, alitumia nafasi hiyo kuzikumbusha kampuni zingine kuiga mfano huo katika kurejesha sehemu ya faida wanayoipata katika kuyasaidia makundi yenye mahitaji kwa kuwa nao wanahitaji faraja kama makundi mengine.

Pia, alisema kuna wakati zao hilo lilishuka thamani nchini lakini kwa sasa limerudi upya kulinganisha na vipindi vilivyopita na Mkwawa inatarajia kununua tani 122 za tumbaku na kuwataka wahakikishe wanapanga madaraja na kutenganisha chafu na safi.




Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, akisaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Sengerema - Nyehunge (km 54.4) kwa kiwango cha lami na Mwakilishi kutoka kampuni ya AVM - Dilingham kwa gharama takribani Bilioni 73 Mkoani Mwanza. Barabara hiyo ni sehemu ya mtandao wa barabara inayounganisha Mkoa wa Mwanza na Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma. **PICHA: WIZARA YA UJENZI**

# Wanaogomea chanjo ya mifugo waonywa

**Na Alex Sayi** MASWA

MKUU wa Wilaya ya Maswa, mkoani Simiyu, Aswege Kaminyoge, amewaonya wafugaji wote wanaogomea utoaji wa chanjo kwa mifugo inayoyoendelea katika kata 36 wilayani hapa.

Amesema, chanjo hiyo ni kwa ajili ya kunusuru mifugo yao na magonjwa mbalimbali ili waendelee kufuga kwa tija.

Kaminyoge alitoa onyo hilo katika kata ya Zanzui na kuwataka wafugaji kutohusisha chanjo hiyo na Kampeni lililositishwa kwa muda na serikali ya kuvisha ng'ombe hereni.

"Wafugaji jitokezeni kuchanja mifugo yenu ili isipatwe na magonjwa na kampeni hii haina uhusiano wowote na uvishaji wa hereni mifugo, hivyo mifugo yote ni lazima ichanjwe," alisema. Pia, aliwataka watendaji wa kata zote kuhakikishe kampeni hiyo inafanyika kwa uwazi kwa kuwashirikisha wafugaji ili kuwapatia taarifa mapema na kuondoa malalamiko ikiwa ni pamoja na maofisa mifugo kutoa vibali kwa wafugaji wataochanja mifugo yao.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Maswa, Onesmo Makota, alisema kampeni hiyo ni takwa la kisheria na imo katika la Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hivyo wafugaji wanapaswa kujitokeza kuchanja mifugo yao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Daktari wa Mifugo wa Wilaya, James Kawamala, alisema kwa mujibu wa takwimu za mifugo za mwaka 2017, halmashauri ina ng'ombe 305,640, Mbuzi 122,256 na kondoo 76,410.

Kwa sasa, alisema chanjo hiyo inahusisha magonjwa mawili ambayo ni homa ya mapafu ya ng'ombe(CBPP) na sotoka ya mbuzi na kondoo kati ya magonjwa 11 ya mifugo. Alisema gharama ya chanjo hizo ni Sh. 800 kwa kila ng'ombe na Sh. 400 kwa kila mbuzi na kondoo.

Ng'wandu Ndoleleji, mkazi na mfugaji wilayani hapa, alishukuru kwa kufikishiwa huduma hiyo karibu huku akiahidi kushiriki kikamilifu kutokana na kutokupata huduma hiyo kwa zaidi ya miaka mitatu huku akiiomba serikali kupunguza gharama za uchanjaji wa mifugo hiyo.

# NHIF yawasajili wanachama 6,481

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Kagera, umesajili wanachama wapya 6,481 kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai, 2022 mpaka Machi, mwaka huu.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Kagera, Mathias Sweya, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza katika mahojiano maalumu na Nipashe.

Alisema, wamefikia hatua hiyo kutokana na hamasa na elimu inayotolewa kwa wananchi kwa lengo la kueleza umuhimu wa kuwa na bima ya afya kabla ya majanga hayajawakuta.

Sweya alisema, mfuko umesajili wanachama kwa kipindi cha miezi tisa kutoka katika taasisi za umma 126, binafsi 922 watu binafsi (vifurushi) 499, wanafunzi 4,187 na watoto chini ya umri miaka 18 ni 747.

Ailiongeza kuwa NHIF mkoani Kagera inaendelea na utoaji wa elimu kupitia makundi ya wafugaji, wakulima na wanafunzi hadi mwananchi mmoja mmoja.

Pia alisema, wako wananchi wanaofika kukata bima pindi wanapokuwa wamefikiwa na ugonjwa unaomhitaji kwenda hospitali kubwa kutibiwa na kuwa na haraka ya kupewa kadi wakati huo hali ambayo si sahihi kwa kuwa bima hizo hukatwa mapema si kwa dharura bali kwa ulinzi wa familia na mwananchi mmoja mmoja.

Alisema familia ikiwa imeandaa bima ya afya kabla majanga, itasaidia hata kutoingiza umasikini kwa kuwa kuna uwezekano wa kuuza mali ili kulipia gharama za matibabu.



Ukurasa 14

'Mahausigeli' walivyoingizwa kwenye semina inayowanoa kwenda sawa na yanayowakuta



Ukurasa 12

Mjasiriamali msomi, awafungua macho kinamama ya teknolojia

Nipashe

TESA

Jumanne Aprili 25, 2023

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

**Kampuni digitali Korea Kusini yaingia ubia na Tume Tehama 'kusafisha' biashara nchini**

ELIMU

NA HALFANI CHUSI

# 'Mtale wa Ngariba', shairi lililompa Mwalimu Amri ushindi, na mamilioni

• Serikali rasmi yasambaza kazi yake shuleni

USIKU wa April 13 uligeuka lulu kwa Amri Abdalah (32), baada ya kuibuka mshindi wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, hali iliyomfanya azoe mamilioni ya shilingi.

Amri aliibuka mshindi kwa kuandika Diwani iliyokuwa mfumo wa simulizi iliyoipa jina la 'Mtale wa Ngariba' ikihusu ukeketaji na madhila ya unyanyasaji yanayowakumba watoto wa jamii ya kimasai.

Kutokana na lugha aliyoitumia na wazo la kipekee kwenye kuwasilisha kazi hiyo, serikali kupitia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Adolf Mkenda, inalazimika kuichukua na kuisambaza maeneo mbalimbali ikiwamo shuleni, maktaba na vyuoni.

Akizungumza katika ofisi za Nipashe hivi karibuni, mshindi huyo anasimulia ameamua kuandika muswada huo, kwa kuwa ni kisa cha kweli na yeye ni shuhuda, hata akaamua kuhamishia kwenye andiko.

"Mtale wa Ngariba, maana yake ni kisu cha Ngariba. Mtale ni neno la Kiswahili lenye maana ya kisu, lakini watu wengi hawautumii msamiati huu, ndio maana nimeutumia ili watu waujue.

"Mimi niliamua kuja na hadithi kwenye miswada yangu na kuipeleka kwenye mashindano, baada ya kukutana na binti wa Kimasai mwaka 2010, aliyekuwa miongoni mwa waliopitia changamoto ya ukeketaji na kulazimishwa kuolewa akiwa na umri mdogo,"anarejea mkasa uliommsukuma kwenye wazo la kuandika hoja hiyo, akiongeza:



Rais Mstaafu wa Msumbiji, Joaquim Chissano (wa pili kulia), akimkabidhi tuzo Amri Abdallah, baada ya kuibuka mshindi wa uandishi bora wa diwani ya shairi. Kushoto ni Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

'Nilipomuhoji kwenye simulizi yake, aliniambia baadaye alipata ujauzito, lakini hakuna aliyekuwa anajali, kwa sababu alitoroka nyumbani kukwepa kuolewa kilazima, akajifungulia porini kwa kuwa hakuna aliyekuwa anamjali.

Amri anasema, baada ya hapo akamchukua na kumpeleka kwa mama yake mdogo, wakawa wanaishi pamoja. Anasema, kitendo hicho kilimuumiza sana na alipoona imetokea nafasi ya kuandika ushairi kwa ajili mashindano, akaamua kutumia kisa hicho ili kupeleka ujumbe kwa jamii" anaeleza Amri, ni mzaliwa wa Kilimanjaro, ambaye sasa ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Baobab, iliyoko Mapinga, Bagamoyo.

Amri, anafafanua kuhusu kisa cha binti huyo wa kimasai (jina tunalo), pia imejikita katika azma ya kumkomboa mwanamke dhidi ya ukatili wa kijinsia, kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kifikra. Mbali na serikali kuchukua jukumu la kukisambaza kitabu hicho kwenye taasisi za elimu, bado Amri anasema ataendelea kunufaika na malipo kutokana na manunuzi kwa wahitaji wa ununuzi wa vitabu hivyo.

"Nina furaha kushinda tuzo hii, ukizingatia ndio mara ya kwanza tangu imeanza hii ni tuzo kubwa Tanzania. Ni heshima kuipata kwa sababu washiriki walikuwa wengi, lakini imekuja kwangu.

"Pia, ninawashukuru majaji wa tuzo hizi wakiongozwa na Jaji Mkuu, Profesa Fiken Senkolo, wamefanya kazi kubwa sana na ndani ya muswada wangu, nimeelezea namna kisu cha ngariba kilivyosababisha kuharibika kwa mfumo mzima wa maisha kwa binti wa kimasai," anasema

### AIPONGEZA SERIKALI

Amri anasema shilingi milioni 10 aliyoipata kama zawadi siku hiyo, inamnufaniha kwa mambo yake mengi ya msingi, huku akiimwagia sifa serikali kwa ubunifu wa kuandaa tuzo hizo.

"Serikali imefungua milango mipya, kwa sababu inawapa wabunifu nafasi ya kuonyesha kile walicho nacho na kuhamasisha wengine kupenda kuandika na kusoma vitabu.

"Jambo zuri zaidi tokea kuanzishwa kwa tuzo hizi, muitikio ulikuwa mkubwa sana, zilipokewa kazi 283, kati yake 79 zilionekana hazijakidhi vigezo kabisa, zikabaki 204 kwenye hizo tena moja ikaonekana haifai ikaondolewa.

"Kwa hiyo, katika kazi 203 zilizobaki 159 zilikuwa za ushairi na riwaya zilikuwa 44. Haya ni mapinduzi na mafanikio makubwa sana kwenye tasnia ya elimu na nchi kiujumla," anasema.

Anafafanua kuwa anasema kazi yake ya ushairi ina beti 314, akisifu ni hadithi tamu inayoburudisha, ambayo mtu anapoanza kuisoma hatotamani kuishia njiani.

Anafafanua uzoefu wake kwenye mashindano ya aina hiyo, akikumbushia aliwahi kushiriki kwenye mashindano ya 'Safal Cornel' yaliyokuwa ya mfumo huo, lakini hakufanikiwa kushinda.

### DHAMIRA IJAYO

Anachoamini, muswada huo umetoa elimu na kuwaasa wazazi umakini kwenye malezi na maadili ya watoto, jamii kuacha kukumbatia mila na desturi zilizopita na wakati, mfano ukeketeji ambao ndio sababu ya binti kuharibikia, kama alivyoisimulia kwenye andiko lake.

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO

# Mjasiriamali msomi, awafungua macho kinamama 'mtatoka kupitia teknolojia'

NI msomi na mjasiriamali. Huyo ni Mkurugenzi wa taasisi inayojishughulisha na kutoa elimu kwa jamii, iitwayo Wezesha Mabadiliko (WEMA) Dk. Lusako Mwakiluma.

Kauli yake ya kitaalamu inasimamia, ni vema wanawake wa Kitanzania wakazitumia teknolojia mpya zilizopo, huku wakibuni na kuanzisha vitu vingi vyenye tija vya kuonekana na kutumika katika ulimwengu mzima.

Dk. Lusako anasema wanawake ni lazima waonyeshe uthubutu katika kutekeleza vitu vingi vilivyopo, sambamba na teknolojia inayokuja kwa kasi, hata ikawafanya wasiwe na hofu ya kufanya mambo makubwa, kwa sababu licha ya kukua teknolojia, bado wapo wanawake wenye woga wa kufanya mambo hayo, hata kuwafanya wawe nyuma kimaendeleo.

Anasema, licha ya baadhi yao wana uwezo kuendesha magari ya kisasa, bodaboda, mabasi ya abiria, meli na hata ndege, sambamba na uthubutu wa kufanya biashara kubwa kama kwenda nchi kama za Uturuki, China na Japan kuchukua bidhaa kwa ajili ya kusogeza mbele gurudumu la maendeleo, lakini wapo ukiwauliza wanasema hawajui hata wafanye biashara gani.

"Ni vema wanawake wengi wakabadilika na kuwa na mitazamo sahihi hasa kwenye masuala a maendeleo, utamkuta mwanamke amekaa nyumbani kuanzia asubuhi hadi jioni bila ya kufanya shughuli yoyote ya kumuongezea kipato, hadi lini mwanamke utaitwa golikipa, ni wakati sasa mwanamke afanye biashara hata tatu au nne ili kuwa na kipato cha uhakika" anasema Dk. Lusako.

Hapo anafafanua kwa mfano binafsi kwamba, yeye akiwa ametunukiwa shahada ya usomi ngazi ya udaktari, bado anaendesha shughuli za kumuongezea maendeleo, zikiwamo za kutoa huduma za kibenki, akiwa ni wakaka wa benki zaidi ya nane, ikiendana na kampuni kadhaa za simu,



Mkurugenzi wa asasi ya WEMA, Dk. Lusako Mwakiluma. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

> Mwanamke jasiri lazima ahakikishe binti yake anakuwa jasiri hata kumzidi yeye katika kutenda kwa kutumia teknolojia zilizopo.

Rai yake kwa kinamamama, waingie katuijka anachokiita 'mioyo ya kuamka', kutenda na kubuni wanachomudu, kwa sababu biashara ziko nyingi, lakini tatizo kubwa lililopo ni wanawake au kinamama ni kuchagua biashara huku wakiwa hawana mitaji ya uhakika.

Dk. Lusako anawaomba wanawake kujenga tabia ya kuwafundisha watoto wao wa kike shughuli za maendeleo, ili waweze kufanya miradi ya maendeleo kama wao na kusimama katika misingi mizuri ya maendeleo kwa kutumia teknolojia zilizopo.

Anasema, mwanamke jasiri lazima ahakikishe binti yake anakuwa jasiri hata kumzidi yeye katika kutenda kwa kutumia teknolojia zilizopo.

"Usiogope kazi ya mtoto wa kiume kumwambia mwanao wa kike aifanye, mfundishe aifanye na ataweza kuifanya kwa kutumia teknolojia kwani itamrahisishia na kuwa mahiri sana, tusiwape kazi laini laini watende kama tunavyopenda na wafanye kama tunavyofanya.

"Sijawahi kuona kuna kazi inanishinda, labda ya kuoa tu, kwa kuwa sio stahiki yetu. Tunatakiwa tuwe chini ya himaya ya mwanaume, pia tuwe watii lakini hatukatazwi kuwasaidia wanaume zetu ili kujenga familia zetu" anasema.

Hata hivyo, anawataka wanawake kuondoa hofu ya kushindwa, bali wafungue viwanda vidogo na vikubwa na kufanya kazi ya kumsaidia Rais Dk. Samia kusimamia majukumu ya kulijenga Taifa.

Aidha, mkurugenzi huyo wa ujasiriamali anaeleza anachoamini kwamba wakitokea wanawake wengine walio tayari kusimama kwa uadilifu na kujituma katika kutumia vyema teknolojia zilizopo kimaendeleo, Rais Dk. Samia atazidi kuwekeza mikopo kwao, pia akiboresha iliyopo kwenye halmashauri nchini.

"Pesa zipo, kila halmashauri na hazina wakopaji. Ukiwakumbusha wanawake kukopa, wanasema hawawezi kuunda vikundi sababu hawaaminiani, jamani tunachelewa wapi?"anang'aka mama huyo.

Anaendelea kunyoosha kidole kuwa: "Adui wa mwanamke ni mwanamke mwenziwe! Hebu wanawake tuwe timu moja, mwenzio akitenda, wewe mbariki na wewe ukitenda yeye atakubariki, hauwezi kutembelea nyota ya mtu hata siku moja."

Hivyo, anawaasa wanawake kupitia teknolojia na usawa wa kijinsia, wasimame kuona kama wataweza kufanya hata yasiyowezekana, lakini yanayofaa kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Dk. Lusako anawataka wanawake kutambua kuwa wanaume ni vichwa ndani ya nyumba hawawezi kushindana nao ila washindane nao kwa fursa na weledi katika kutenda kwa sababu anasema mume mwema akiona mke wake anapambana atashukuru na kuona anaisaidia familia yake kuinuka naye atapata nguvu zaidi.

## 'Mtale wa Ngariba', shairi lililompa Mwalimu Amri ushindi na mamilioni

**INATOKA UK.11**

Dhamira nyingine anaitaja ni kuwataka wanawake wasijibeze na kwamba wanaweza kufanya shughuli yoyote, kama ilivyo kwa wanaume, kikubwa ni wazazi kuwa makini kwenye malezi ya watoto na watu wa karibu, haki ya mtoto kupata elimu na muhimu ni penye elimu ya jinsia na maadili, kuanzia ngazi ya msingi.

Mshindi huyo anawasihi wadau wengine kujitokeza kushiriki tuzo hizo kwa mwaka ujao, kwa kuwa hazina mipaka na hazichagui watu wa kuwania.

"Milango ya kushiriki ipo wazi kwa mtu yeyote, japo kwa mwakani walisema wataongeza baadhi ya vipengele, sio riwaya na ushairi pekee kama ilivyokuwa mwaka huu, itakuwapo pia tamthilia, hadithi fupi, fasihi ya watoto na tafsiri," anaeleza mtaalamu huyo wa ushairi.

Anashauri kwa yeyote anayeweza kuandika, wakati ni sasa kwa kuwa lugha ya kiswahili imeenea zaidi nchi jirani na serikali ipo kwenye mpango wa kuifikisha mbali zaidi lugha hiyo.

Anasema kwa mtu, anayetaka kushiriki kwaajili ya tuzo ahakikishe anafuata maelekezo yaliyotolewa na tume ya tuzo, pia andiko lake liguse masuala ya kijamii na liwe makini kwenye ubunifu wa hali ya juu na lugha rafiki itakayo mshawishi msomaji kusoma na kumaliza kitabu kizima.

### SIRI YA MAFANIKIO

Pamoja na uzuri wa kazi yake,Abdala anataja siri ya mafanikio yake Kwamba wapo waliomshika mkono na kushirikiana nao mpaka kuibuka mshindi tuzo hiyo.

Anataja mafanikio yake, ni zao la kumtanguliza Mungu mbele na ushirikiano alioupata kutoka kwa walimu wenzake na familia yake kwa ujumla.

"Ninaishukuru serikali, ya Rais Samia Suluhu Hassani kwa kukubali kutoa fedha kiasi cha bilioni moja na zaidi, kwaajili ya tuzo hizi, pia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) iliyopewa jukumu la kusimamia tuzo hizo kupitia Mkurugenzi wake, Aneth Komba.

"Pia uratibu mzuri uliofanywa na kamati ya tuzo chini ya Prof Penina Mlama, ambaye ndiye alikuwa Mwenyekiti wa Tuzo hizo, pamoja na majaji," anasema.

TEKNOLOJIA

NA BEATRICE PHILEMON

# Kampuni digitali Korea Kusini, yaingia ubia na Tume Tehama 'kusafisha' biashara nchini

HIVI karibuni Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, imeingia mkataba wa kisheria na kampuni ya Aron Group, ya Korea ikitarajiwa itaunganishwa na mifumo ya serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, anasema ni hatua itakayoisaidia serikali nchini kuongeza pato la taifa na wakati huo huo, kusaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati kuwa na historia nzuri ya biashara zao, hatimaye kupata mikopo kutoka kwenye benki au taasisi za kifedha.

Lingine linatajwa katika hoja hiyo, ni kwamba mkataba utaleta chachu kubwa katika sekta ya TEHEMA nchini, ikiboresha kutoka sekta isiyo rasmi kuwa sekta rasmi, vilevile kukiletwa teknolojia ya kisasa nchini, kutoka Korea Kusini.

Kampuni ya Aron Group ni kampuni, ina makao makuu nchini Korea Kusini na hivi sasa imefungua tawi nchini Tanzania kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo na kati kutumia njia ya kidigitali katika biashara zao hasa malipo na huduma nyingine.

Dk. Mwasaga anasema kuwa katika utekelezaj, kampuni ya Aron Group itaunganishwa na mifumo ya kiserikali, hapa akifafanua "itafanya kazi yao vizuri au kutoa huduma nzuri kwa wananchi wa Tanzania, itawavutia wawekezaji wengi zaidi kutoka Korea Kusini kuja kuwekeza nchini."



ofisa Mtendaji wa kampuni ya Aron group Tanzania, Taegyun Kim, wakibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini, Dk. Nkundwe Mwasaga, mara baada ya kutia saini mkataba wa makubaliano. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

Anasema, ili kuhakikisha Tanzania inakuwa shindani katika uchumi wa kidigitali, tume yake inahakikisha wanatoa huduma inayokidhi haja ya kusaidia serikali, kwa kupata kodi kupitia miamala ya simu.

"Lengo kuu la kuwezesha kampuni hizi tunataka zikue na kupeleka huduma nchi jirani, watoe ajira Tanzania na nchi jirani na pia tunataka Tanzania ijulikane ina uchumi wa kidigitali na isaidie kuleta teknolojia ya kisasa," anasema.

Kwa mujibu wa bosi huyo wa Tume ya TEHAMA, kampuni hiyo mbia wa teknolojia, inalenga kuisaidia serikali kujua idadi ya wafanyabiashara walioko nchini, hata kukawapo takwimu sahihi kuhusu kiasi cha malipo (transactions) kinachofanyika kwa siku au mwezi kupitia mitandao ya simu.

"Sisi kama tume katika kukuza na kutafuta njia ya kuvutia watu na wawekezaji, pia tunashiriki kwenye makongamano makubwa nje ya nchi. Pia, Tanzania ina kongamano lake ambalo linakutanisha wadau mbalimbali waliopo kwenye sekta ya TEHEMA," anafafanua.

Tume ya TEHAMA hadi sasa inaelezwa inatoa mafunzo ya muda mfupi kwa watalaamu wa sekta hiyo, pia wanawatafutia wadau wengine wanaoweza kutoa mafunzo ya muda mrefu, ili kutoa huduma nzuri ya fani hiyo, wataalamu wazuri wanaoaminika, pia kwenye kanzi data ya taifa.

Anasema, hadi sasa tume ya Tehama imefanikiwa kusajili kampuni zaidi ya 300 (Start-up companies) na zinatakiwa zitoe huduma katika nchi ya Tanzania, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ma Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC), mtazamo wa kiufundi ulioko ni kuwapo uchumi wa kidigitali nchi nzima.

**HATUA ILIYOFIKIWA**

Dk. Mwasaga anasema hadi Tume ya TEHAMA imeshafanikiwa kusajili wataalamu wake 1600 na sasa inaangalia uwezekano wa kufanya nao kazi, pia kuwapa mafunzo ya muda mfupi, akitaja msimamo wake kwa sasa ni kwamba, wanauunga mkono taasisi changa za TEHAMA zinazochipukia, ili ziwe chachu katika utoaji ajira kwa vijana na kurahisisha utoaji huduma nchini na mataifa jirani.

"Tutaendelea kuhakikisha upatikanaji huduma za kidigitali katika mifumo ya miamala ya pesa inakuwa ya uhakika na yenye kukidhi usalama wa pesa za mtumiaji," anasema

> Mfumo huu ni salama na rahisi kwa mtumiaji, imekidhi vigezo nawaomba Watanzania hasa wafanyabiashara hapa nchini kutumia mfumo huu.

Anataja takwimu kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), ni kwamba kuna jumla ya kampuni ndogo milioni 30 zinazotoa huduma kwa 'cash' na hazina rekodi ya biashara wanazoifanya.

"Sisi kama tume (ya TEHAMA), tunapenda huduma zote zinazotolewa na kampuni hizi zianze kutolewa kwa njia ya mtandao, ili kuwasaidia kuwa na rekodi sahihi kuhusu biashara zao na malipo ya biashara zao," anasema na kuongeza kuwa "kampuni nyingi zinaanzia watu wanne na kuendelea."

Pia, anatoa rai kwa kampuni nyinginezo kuja kuwekeza Tanzania katika sekta ya TEHAMA kwa sabau serikali ya Tanzania kupitia tume ya tehema imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji .

**ARON GROUP**

Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Aron Group, Leonce Mongi, akizungumza na Nipashe, anasema hadi sasa kampuni yake imetengeneza mfumo wa malipo unaoitwa 'shake up' na 'digital payment solution' zikiwa mahsusi kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati, kupokea malipo kutoka kwa wateja wao, kupitia simu za mkononi.

Kupitia mfumo huo wa 'shake app' anadems mfanyabiashara ataweza kutangaza biashara zake, pia mfumo huo utawasaidia wafanyabiashara kukusanya taarifa za mapato na matumizi kupitia mfumo huu, hivyo kuwa na historia nzuri ya miamala wanayofanya katika biashara zao au huduma wanazozitoa katika maeneo yao.

"Mfumo huu ni salama na rahisi kwa mtumiaji, imekidhi vigezo nawaomba Watanzania hasa wafanyabiashara hapa nchini kutumia mfumo huu," anausifu ubunifui huo.

Kwa mujibu wa Mongi, Aron Group hivi sasa imefunga ofisi zake Dar es Salaam, lakini baada ya miezi sita itapeleka huduma zake katika mikoa mbalimbali nchini.

"Tumeamua kujikita katika eneo hili baada ya kugundua kuwa wafanyabiashara wengi wametawaliwa na sekta isiyo rasmi, sisi kama kampuni tumekuja na mfumo huu kusaidia serikali kujua kuna wafanyabiashara wangapi hapa nchini, miamala mingapi inafanyika kwa siku, mwezi na tutaendelea kuwa pamoja na serikali na tunashukuru Tume ya Tehema kwa kusaini mkataba na sisi," anasema.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# 'Mahausigeli' walivyoingizwa kwenye semina inayowanoa kwenda sawa na yanayowakuta



'Wadada wa kazi' wakiwa mafunzoni katika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

KUNA baadhi ya wafanyakazi majumbani wanakiri kupitia unyanyasaji wa aina mbalimbali, ikiwamo mashambulio ya aibu, ngono na mateso mengineyo ya hatari kwa afya zao, kwani seketa hiyo imetawaliwa na mabinti wenye umri chini ya miaka 18 katika umaarufu wao 'wadada wa kazi' au 'wasichana wa kazi.'

Hata hivyo, inaelezwa taarifa nyingi za idadi yao majumbani katika kaya, hazipatikani kirahisi kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo waajiri kutokuwa tayari kuweka wazi. Ni haki inayoifanya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam, kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa malezi na makuzi wafanyakazi hao mkoani Dar es Salaam, ili wajitambue haki zao, kuepuka mazingira yanayowagusa.

Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Joyce Nyoni anasema miaka ya karibuni kumekuwapo kelele nyingi za malalamiko kuhusu malezi na tabia za watoto, hivyo wanaamua kutoa mafunzo kwa wasaidizi hao 100 wa majumbani.

"Kinamama wengi wanaondoka asubuhi na kurudi jioni, watoto wao wanakaa na 'madada wa kazi', lakini bahati mbaya hawana uelewa kuhusu malezi na makuzi ingawa wana mchango mkubwa katika kulea," anasema Dk. Joyce.

Pia, anafafanua ni mchakato ambao 'madada wa kazi' nao kuna siku watakuwa mama, hivyo ni muhimu wakaelewa wanavyopaswa kulea mtoto, kulingana na mabadiliko yaliyoko.

### WALIVYONOLEWA DARASANI

Dk. Joyce anafafanua walichokifanya, ni kuwajengea uwezo watambue na kuepuka unyanyasaji unaoweza kuwakumba, ukiwamo wa kingono ambao ni hatari kwa afya zao.

Anasema uelewa unamsaidia mtu kujitambua, pia kutambua hatari, hata akaepuka, akimini mafunzo hayo ya watumishi, yatawafanya kuwa mabalozi azuri waliko majumbani.

Anafafanua kwamba, wakati ukatili unatokea, 'wadada' hawawaelewi watoto na kwamba wakimuelewa, watajua namna ya kuwasaidia, mabosi nao wawafanye wawe katika mazingira ya kujiamini anapolea mtoto.

"Ni mafunzo yaliyoambatana elimu ya jinsi ya kukabiliana na misongo ya mawazo, matumizi sahihi ya fedha na kuweka akiba, usafi pamoja na mawasiliano kwa mabosi wao. Ni namna inahuisha hisia ya kutoweza kukabiliana na mahitaji yanayotokana na kazi, mahusiano, shinikizo za kifedha na hali nyingine za maisha. Sisi sote tunapitia msongo wa mawazo kwa njia tofauti," anasema.

Anafafanua kwamba, mara nyingi mtu anaweza kushindwa kujua kuwa anachopitia ni msongo wa mawazo na kwamba, akiwa anapata mabadiliko hayo, kuna uwezekano kuwa anakabiliwa na msongo wa mawazo.

Kwa mujibu wa Dk. Nyoni, msongo wa mawazo unaweza kumsababisha mtu akapoteza hamu na tamaa ya kufanya alichokuwa akifurahia awali, akihisi kufa moyo au kukosa tumaini akitawaliwa na hisia mbaya, binafsi akitafsiri 'amefeli' maisha.

"Tumeona ni muhimu tuwape elimu watambue hayo, kutokana na ukweli kwamba wanapitia changamoto nyingi ambazo wakati mwingine husababisha wafanye ukatili kwa watoto wa mabosi wao," anasema.

Mhadhiri wa taasisi hiyo na Mratibu wa Kitengo Ushiriki Jamii, Dunstan Haule aliyeshitriki kufundisha mafunzo hayo, anasema yatawasaidia katika usafi, kujilinda na namna ya kuwasiliana pale wanapokuwa na changamoto ndani ya familia.

"Pia, upande wa akiba, ninaamini mafunzo waliopata yatawasaidia kutambua umuhimu wa kujiwekea akiba benki, kwa ajili ya maisha yao ya baadaye na sio kutumia fedha yote ya mshahara," anasema Haule.

### WANUFAIKA WANENA

Lucy Lazer, ni mnufaika wa mafunzo hayo, anayeeleza amejifunza namna ya kuepuka unyanyasaji kingono, kukaa na watoto na kucheza nao, hata kutambua mabadiliko katika makuzi yao.

"Nitakwenda kutumia mafunzo haya kwa vitendo, ili kufanya kazi yangu kwa ufanisi zaidi kule ninakoishi, kwani nimejifunza mengi, hasa namna ambavyo nitaweza kuepuka unyanyasaji kukaa na watoto," anasema Lucy.

Mnufaika mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Martha Kavindi, anaeleza imani yake kwamba, mafunzo yatamjengea uwezo wa kulea watoto wa mabosi wao vizuri na hata wao wenyewe kujiandaa kuwa mama wa baadaye.

"Ni wazi kwamba kila mmoja wetu amejua hatua za ukuaji wa mtoto kimwili, kiakili, kiroho na ukuaji wa kijamii na amejua watoto anaowalea wanapitia hatua zote kama tulivyofundishwa," anasema Martha.

Mshiriki ambaye ni mfanyakazi wa ndani na hakupenda jina lake kuandikwa gazetini, anakiri wanapitia changamoto nyingi, ikiwamo wazazi wa watoto kutotoa nafasi ya kuwasikiliza, hali anayodai inayowachosha.

"Tunashindwa kueleza changamoto walizonazo watoto wao katika makuzi, yaani wazazi wana majukumu mengi wanakosa nafasi ya kuwasiliana nasi," anasema.

## WANENAVYO MALENGA

### MAMA MKWE KIVURUGE

Mama mkwe kivuruge, huyo ni hasara kubwa,
Ni sawa na kula zege, na wala siyo ubwabwa,
Nyumba aleta matege, na hata vurugu kubwa,
Mama mkwe mkorofi, ni bora kumuepuka.

Mama mkwe mkorofi, ni bora kumuepuka,
Utasema mbona hafi, uweze kupumzika,
Sawa na bidhaa ghafi, haifai kutumika,
Akija ni tumbo joto, amani inatoweka.

Akija ni tumbo joto, amani inatoweka,
Jinsi anawasha moto, yake mwanae ashika,
Linatawala fukuto, hadi atapoondoka,
Amri nyumbani kwake, ndizo zinahamishika.

Amri nyumbani kwake, ndizo zinahamishika,
Ndoa yenu yawa yake, afanya analotaka,
Yadumu mipango yake, yenu chini anaweka,
Kuoa na kuolewa, kunakuwa kuteseka.

Kuoa na kuolewa, kunakuwa kuteseka,
Yake ndiyo yaenziwa, hata kutekelezeka,
Ya mwenza yanafukiwa, hata ya kueleweka,
Kuja kwake wajutia, badala kushereheka.

Kuja kwake wajutia, badala kushereheka,
Aja unafikiria, ni lini ataondoka,
Ili yako familia, ipate stareheka,
Mama mkwe huyo zigo, gumu sana kubebeka.

Mama mkwe huyo zigo, gumu sana kubebeka,
Tena huyo ni kigogo, kwa mwanaye apendeka,
Lazima uweke logo, ya kwake kuvumilika,
Akisema hakutaki, ndoa yaweza vunjika.

Akisema hakutaki, ndoa yaweza vunjika,
Yake kwa mwanaye tiki, ndiyo yanaaminika,
Tamani akulaiki, usibaki takataka,
Mama ni mvunja ndoa, pia aweza simika.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



# TARI yazindua vituo usambazaji teknolojia

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imezindua vituo vinne vya kusambaza teknolojia ili kuhakikisha matokeo ya utafiti yanaleta mabadiliko chanya katika sekta ya kilimo.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema jana kuwa vituo hivyo ni vya Nyakabindi (Simiyu), Nzuguni (Dodoma), Fatma Mwassa (Tabora) na Mwalimu Julius Nyerere kilichoko Morogoro.

Alisema, ili kuhakikisha matokeo ya utafiti yanaleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya kilimo nchini, TARI imepeleka matokeo ya utafiti mbalimbali kwa wadau 5,497,547 wakiwamo wakulima na maofisa.

Dk. Mkamilo alisema njia zilizotumika kusambaza teknolojia hizo ni pamoja na maonyesho mbalimbali ya wakulima, sikukuu za wakulima, maonyesho ya kilimo biashara, mafunzo wezeshi, majukwaa bunifu na mashamba darasa yaliyoko katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi huyo alisema wakulima wameelimishwa kukusu matumizi sahihi ya teknolojia hizo zinazolenga kuongeza uzalishaji na tija katika uzalishaji mazao ya kilimo.

"Tumekuwa tukitumia njia hizo kwa ajili ya kusambaza teknolojia mbalimbali za kilimo kwa wakulima, lengo ni kila mmoja ajue na kuendesha kilimo chenye tija," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mkamilo, licha ya kusambaza teknolojia hizo bunifu, taasisi imeendelea na miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu muhimu ili kuongeza ufanisi wa utafiti inaofanya.

Pia alisema, alisema katika jitihada za kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za mazao nchini, TARI imeendelea kuboresha miundombinu ya utafiti na uzalishaji. Katika kipindi cha miaka miwili, alisema maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yamefanyika kwenye eneo la hekta 854 katika vituo 16 vya utafiti.

Alisema, kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo, kutawezesha uzalishaji wa mbegu na majaribio ya utafiti kufanyika mwaka mzima.

"Tuko pia katika hatua nzuri ya ujenzi wa maghala matano ya kuhifadhia mbegu yenye vyumba vya ubaridi katika vituo vya TARI Naliendele, Tumbi, Hombolo, Seliani na TARI Dakawa, mradi ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 10," Dk. Mkamilo.

Pia alisema, ili kulinda maeneo ya utafiti dhidi ya uvamizi, TARI imekamilisha maandalizi ya kumpata mzabuni atakayeanza ujenzi wa uzio katika eneo la TARI Uyole lenye ukubwa wa hekta 1,042.



Spika wa Bunge Dk Tulia Ackson (kulia) akijadiliana jambo na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ,Abdalah Ulega walipokutana ndani ya ukumbi wa Bunge Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Bilioni 6/- kukamilisha ujenzi shule Dodoma

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema zaidi ya Sh. bilioni sita zimetengwa ili kukamilisha ujenzi wa shule mpya za msingi 16 katika mkoa.

Senyamule aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika kikao cha kujadili mradi wa BOOST na wakuu wa wilaya, maofisa elimu na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa kilichofanyika ofisini kwake.

Alisema vyumba vya madarasa 153 vitajengwa na zaidi ya Sh. bilioni tatu zimetengwa kuhakikisha vinakamilika.

"Madarasa ya mfano elimu ya awali 16 yatajengwa na Sh. milioni 508.8 zimetengwa, darasa la elimu maalum moja litajengwa na limetengewa Sh. milioni 23 pamoja na matundu 106 ya vyoo yakitarajiwa kujengwa kwa Sh. milioni 180.2," alisema.

Pia alisema kupitia mradi wa SEQUIP, zaidi ya Sh. bilioni tano zilipokewa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 11 za sekondari na kila shule ilipata zaidi ya Sh. milioni nne kwa shule za Mpingwa (Bahi), Mtemi Chiloloma (Dodoma), Keikei (Kondoa DC), Tura Day (Kondoa Mji), na Lenjulu (Kongwa) na ujenzi wake umekamilika.

Alisema mradi huo ni wa mwaka 2021/22 na ujenzi bado unaendelea kwa shule za Lwondo (Mpwapwa), Zajilwa (Chamwino), Nhinhi (Chamwino) na Churuku (Chemba) huku ukiwa bado unahitaji usimamizi wa karibu ili ukamilike.

# Singida kusherehekea Muungano kwa usafi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKOA wa Singida umepanga kutumia sherehe za miaka 59 ya Muungano kwa kufanya usafi katika maeneo yote ya mkoa ikiwamo barabara kuu ya Singida - Mwanza.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema usafi huo ambao utawashirikisha wananchi pia utafanyika katika ofisi za serikali, taasisi mbalimbali na maeneo ya shule, vyuo na masoko.

Alisema kazi zingine zitakazofanyika ni uzinduzi wa miradi ya maendeleo katika hospitali ya wilaya ya Manyoni hususani jengo la wagonjwa la dharura na kutembelea mradi wa ujenzi wa daraja katika barabara ya Kintinku - Singida hadi Malendi.


Serukamba alitaja shughuli zingine zitakazofanyika ni kufanya mdahalo kuhusu Muungano, kufanya bonanza la michezo, kufanya mahojiano na wazee maarufu wanaojua historia ya mkoa wa Singida kuwaeleza wananchi mafanikio ya maendeleo ndani ya Muungano.

Alisema, katika miaka 59 ya Muungano, kumekuwa na mafanikio mengi kwa wananchi wa pande zote za Muungano yakiwamo ulinzi na usalama, kisiasa na mwingiliano wa kijamii.

Mkuu huyo wa mkoa alisema suala la ulinzi limefanikiwa kwa asilimia 100 hasa ulinzi wa mipaka ya nchi hali ambayo imesaidia kupiga hatua kwenye maeneo ya kijamii, kisiasa na uhusiano wa kimataifa.

"Kama si Muungano wetu, eneo la ulinzi na usalama lingekuwa na changamoto nyingi tofauti na sasa. Jeshi letu la ulinzi ni moja kwa pande zote na hali hii imeleta utulivu na uimara wa jamii zote mbili za Muungano," alisema.

Serukamba alisema katika suala la kisiasa, nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikijifunza Tanzania hasa katika suala la makabidhiano ya madaraka kutoka awamu ya kwanza hadi ya sita bila vurugu tofauti na nchi zingine.





# Wanafunzi kunufaika mafunzo kwa vitendo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Olomitu iliyoko Kata ya Mlangarini, katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, wanaosoma masomo ya sayansi watanufaika kwa kujifunza kwa vitendo baada ya kutolewa Sh. milioni 58 kwa ajili ya kukamilisha jengo la maabara.

Ujenzi wa maabara hiyo ni mkakati wa serikali wa uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi kwa vitendo wanaosoma masomo ya sayansi kwa shule zote za sekondari za serikali.

Jengo la maabara hiyo lilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi kwa Sh. milioni 17 huku halmashauri ikitoa Sh. milioni 30 kupitia mapato yake ya ndani, hivyo kufikisha jumla ya Sh. milioni 47.

Akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la ujenzi wa mradi huo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mlangarini, John Laizer, alisema Sh. milioni 17 zilizochangwa na wananchi zimejumuisha ujenzi wa msingi wa jengo hilo, kupandisha kuta za jengo lenye ofisi ya walimu na chumba cha vitendanishi vya kemikali.

Laizer alisema Sh. milioni 30 zilizotolewa na halmashauri, zimetumika kutengeneza miundombinu ya ndani ya maabara na kupiga plasta.

Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Arusha, Sharif Said, alisema hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 80 na matarajio yao baada ya kumamilika kwa kazi zote, utagharimu Sh. milioni 58.

Alisema, uchangiaji wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaleta tija na uwezo wa kujiletea maendeleo wenyewe badala ya kuitegemea serikali na wafadhili.

Olomitu ni miongoni mwa shule mpya za sekondari na ilianzishwa mwaka huu baada ya ujenzi wa vyumba vya madarasa mawili mwishoni mwa mwaka 2021 kupitia fedha za mapambano dhidi ya UVIKO-19.



Mkuu wa wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Juma Irando akipanda mti jana katika zoezi la upandaji miti ya kutunza mazingira kiwilaya kuelekea kilele cha siku ya Muungano iliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Chatuu wilayani hapa ambapo Afisa misitu wilaya hiyo Obadia Msemo alisema kuwa miti 2000 imepandwa na lengo mwaka huu kupanda miti Milioni 1.5. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Tanzania yapongezwa mafanikio chanjo

**Na Cynthia Mwilolezi**
BABATI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeipongeza Tanzania kwa kupiga hatua katika utoaji wa chanjo mbalimbali, ambazo zimesaidia kutokomeza baadhi ya magonjwa yakiwamo ndui na polio.

Pongezi hizo zilitolewa jana mjini hapa na Ofisa Afya ya Watoto na Chanjo kutoka WHO Tanzania, Dk. Nemes Iriya, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Chanjo Duniani, ambayo kitaifa yanaadhimishwa wilayani hapa.

Dk. Iriya alisema Tanzania imekuwa kinara wa chanjo kwa nchi zinazoendelea kutokana na kuingiza mpango wa chanjo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kila baada ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa Dk. Iriya, mwaka 2012 Tanzania ilithibitishwa rasmi kuwa imefanikiwa kuondoa ugonjwa wa poli, pia kisa cha mwisho cha mgonjwa wa polio nchini kiliripotiwa mwaka 1996. Tangu kipindi hicho, alisema hakutokea mgonjwa wa polio na Novemba, 2015 Tanzania ilitangazwa kuwa imefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo.

"Tunaipongeza Tanzania kwa kuwa imekuwa kinara wa utoaji wa chanjo katika nchi zinazoendelea. Hii inatokana na Ilani ya CCM ya kila baada ya miaka mitano. Kwa sasa magonjwa kama ndui na polio kwa Tanzania hayapo tena na sasa serikali kwa kushirikiana na WHO, magonjwa mengine yako ukingoni kutokomezwa, "alisema.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, mafanikio hayo yanatokana na WHO kushirikiana na serikali kufanya maboresho ya chanjo, kutoa utaalam, miongozo ya sekta ya afya, ubunifu uhamasishaji wa jamii.

Alisema mwitikio mkubwa umesaidia kuongezeka kwa chanjo, kutokomeza baadhi ya magonjwa yanayoweza kuzuilika kwa njia hiyo na kuanzia mwaka 2000 waliwapatia chanjo mbalimbali asilimia 90 ya watoto wote nchini, ikiwamo kwa njia ya mkoba kwa watoto waliko umbali wa kilimita tano kutoka kwenye huduma za afya.

"Tangu WHO ianze kufanya kazi mwaka 1975 tulifanikiwa kuanzisha mpango wa chanjo wa taifa (EPI) ambao ulianza na atijeni mbili, ila kutokana na mwitikio wa jamii sasa hivi Tanzania inatoa antijeni 13 na aina nane za mchanganyiko wa chanjo ambazo zimesaidia kutokomeza baadhi ya magonjwa na nyingine kuisadia wananchi kutopata maambukizi ya magonjwa yanayoweza kudhibitiwa kwa njia ya chanjo," alisema.

Pia alisema magonjwa ambayo kwa sasa yako kwenye mchakato wa kutokomezwa ni na surua kwa kuwa mlipuko wake uko kwa kiasi kidogo tofauti na awali kwa kuwa hata sasa wodi za wagonjwa hao zilishafungwa. Alisema hiyo inatokana na mwamko kwa jamii pamoja na ugonjwa wa pepo punda ambao chanjo zinatolewa kwa wajawazito na watoto wachanga.

Naye Ofisa Ufuatiliaji wa Magonjwa yanayozuilika kwa Chanjo kutoka WHO Tanzaniza, Dk. Boniphace Mwakilemo, alisema hali ya mwamko kwa wananchi ni kubwa na kwa chanjo ya UVIKO-19 asilimia 90 ya makundi maalum walishachanja na nchi zingine bado ni tatizo hata kwa chanjo za kawaida.

# Mwekezaji kusaidia kutatua kero shule

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

KAMPUNI ya Franone Mining Ltd, inayojishughulisha na uchimbaji wa tanzanite, imesema itahakikisha inasaidia kutatua matatizo yanayoikabili shule ya Sekondari ya Naisinyai,iliyoko wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Msaada huo ni pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ya elimu itakayogharimu Sh. milioni 38 katika shule hiyo.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Onesmo Mbise, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza kwenye mahafali ya kwanza ya kidato cha sita ya shule hiyo ambapo alikuwa mgeni rasmi.

Mkurugenzi huyo alisema kamapuni hiyo itasaidia kutatua matatizo aliyoahidi baada ya kukutana na wakurugenzi wenza wa kampuni, Vitus Ndakize na Francis Matunda.

Alitaja baadhi ya matatizo yanayoikabili shule hiyo ambayo kampuni hiyo itasaidia kutatua ni pamoja na kuchimba kisima, umeme wa nyumba, ujenzi wa bweni la wasichana, bwalo na jiko la kudumu kwa kuwa lililopo linaingiza vumbi na kuchafua chakula.

Pia alisema, utaratibu na kanuni za kusaidia jamii iliyoko pembeni ya uwekezaji (CSR), umebadilika kwa kuwa sasa mkurugenzi wa halmashauri hiyo ndiye anapendekeza eneo tofauti na awali.

"Sasa hivi unaweza kuwekeza Naisinyai au Mirerani ila mkurugenzi wa halmashauri akachagua kata nyingine ya kutekeleza CSR ilimradi mradi uko Simanjiro," alisema Mbise.

Aliwapongeza walimu na wanafunzi wa shule ya sekondari Naisinyai ambayo ni miongoni mwa shule za awali za Kata wilayani humo zilizozalisha wasomi wengi.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Naisinyai, William Ombay, alimshukuru mwekezaji huyo mzawa kupitia kampuni yake kuahidi kutatua baadhi ya matatizo yanayoikabili shule hiyo.

Naye Diwani wa Naisinyai, Taiko Laizer, alisema watampa ushirikiano wa kutosha mwekezaji huyo kupitia kampuni hiyo ambayo inajishughulisha na uchimbaji wa tanzanite.



## Sekta ya uvuvi kuimarishwa miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea na mikakati yake ya ushirikiano na washirika wa maendeleo katika kuimarisha sekta ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini katika ujenzi wa miundombinu.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi , Masoud Makame Suleiman aliyaeleza hayo katika hafla ya utambulisho wa mradi wa ujenzi wa Chumba cha mfano cha baridi kitakachotumia nishati ya umeme wa jua pamoja na utiaji saini wa hati ya ushirikiano na kufanya stadi ya kutekeleza mradi wa ufugaji kamba baina ya wizara hiyo na Kampuni ya Last Aple Tree iliyofanyika wizarani kwake, Maisara.

Alisema kwa matukio mawili hayo muhimu ni fursa kubwa kwa maendeleo ya sekta ya uchumi wa buluu nchini.

Alisema wizara yake kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), inakusudia kuendeleza sekta ya uvuvi na kuongeza ufanisi katika mnyororo wa thamani wa samaki na mazao mingine ya baharini. Alisema mradi huo unatarajiwa kutumia teknolojia ya kisasa ya Biofloc Waste Water katika ufugaji wa kamba na kupunguza kwa kiwango kikubwa uchafuzi wa mazingira.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Aboud Suleiman Jumbe, alisema matumizi ya mradi huo yatapunguza matumizi ya umeme na kuongeza ufanisi katika ubora wa samaki na masoko pamoja na kipato.

Hata hivyo, alisema mradi huo unatarajia kuleta tija kubwa katika kipato cha wavuvi na wafugaji kwa kuweka mfumo wa ufugaji ambao mfugaji mmoja atapata kipato cha Dola za Kimarekani 1,000 kwa mwezi.

Mkurugenzi wa ZAFICO, Dk. Ameir Haidar Mshenga, alisema kuwapo kwa vyumba vya baridi, wavuvi watahifadhi samaki na watakuwa na ubora wake.

# Serikali yapitia Sheria ya Mtoto kumlinda udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema wiraza hiyo imeshaipitia Sheria ya Mtoto ya Zanzibar ili kuhakikisha inaendelea kumlinda mtoto na vitendo vyote vya udhalilishaji.

Waziri Pembe aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe Mjini Zanzibar, kutokana na mijadala kutoka kwa baadhi ya watu kuwa umri wa mtoto upunguzwe badala ya mtoto kutambuliwa kisheria kuwa chini ya miaka 18 kwamba sheria hiyo ifanyiwe marekebisho na umri wa mtoto uwe chini ya miaka 14.

"Wapo wanaotaka kuwa umri wa mtoto upunguzwe wakidai kuwa idadi ya watoto wingi wanaozalilishwa ni wasichana kuazia miaka 14 hadi 18 huku wakisema kuwa watoto hao hujipeleka wenyewe kwa wanaume," alisema.

Waziri Pembe ametafautiana na maoni ya watu hao na kusema kuwa umri wa mtoto utabaki kama ulivyoeleza katika Sheria ya Mtoto kwa sababu mtoto chini ya miaka 18 bado huwa hajajitambua.

Alisema endapo umri wa mtoto utapunguzwa, watoto wa kike wataendelea kudhalilishwa na wadhalilishaji kuwapa mwanya.

"Watoto wote walio chini ya umri wa miaka 18 bado wana haki na nafasi ya kulindwa na katika hili serikali inaendelea kuwalinda kwa nguvu zake zote," alisema Waziri Pembe.

Alisema serikali inashirikiana na wadau mbalimbali katika kupinga vitendo vya udhalilishaji na kuwalinda wanawake na watoto na vitendo hivyo.

Pembe, aliitaka jamii yote kusimama pamoja kuwalinda watoto wa jinsia zote maana watoto wote wanadhalilishwa na kwa sasa wimbi kubwa lipo kwa watoto wa kiume.

Hata hivyo alisema lazima kuwapo kwa ushirikiano wa pamoja katika kutokomeza vitendo hivyo maana serikali pekee haiwezi kumaliza tatizo hilo.

"Tupambane katika kutokomeza ushoga, usagaji na vitendo vyote vya udhalilishaji kwa sababu bado baadhi ya watu wanaendelea kutukandamiza kwa kuunga mkono vitendo hivi ambavyo ni kinyume na maadili," alisema.

Kwa mujibu wa takwimu za udhalilishaji kwa mwezi wa Machi mwaka huu kutoka ofisini ya mtakwimu mkuu wa serikali, matukio 155 ya udhalilishaji yameripotiwa Zanzibar.

Katika matukio hayo 155 yaliyoripotiwa ya ubakaji ni 69 na ulawiti 29 na kuingilia kinyume na maumbile matukio sita na waathirika washichana waliobakwa ni 65, wavulana waliolawitiwa 24 na wasichana watano wameingiliwa kinyume na maumbile.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdalla, akikata utepe kuashiria Ufunguzi Jengo la Ofisi ya Makamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja lililopo Tunguu Zanzibar ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Vyombo vya ulinzi kuboreshwa utendaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali zote mbili zitaendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuboresha utendaji wao katika kusimamia usalama wa raia na mali zao.

Alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na kuenzi fikra na mawazo ya waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, hayati Mwalimu Nyerere na Hayati Abeid Karume.

Hemed aliyasema hayo jana katika ufunguzi wa Ofisi ya Makamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini unguja huko Mahonda na Mkoa wa Kusini Unguja lililopo Tunguu Zanzibar ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hafla iliyofanyika Tunguu, mkoa wa kusini unguja.

Hemed alisema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unatokana na nia thabiti ya viongozi hao ambao ni waasisi wa taifa kwa kuzingatia uhusiano wa muda mrefu wa wananchi wa pande zote mbili.

Alisema Muungano huo unabaki kuwa wa kipekee Afrika na duniani kote na kuwataka wananchi kuendelea kuuenzi Muungano huo, kuutunza na kuulinda ambayo ni tunu moja wapo inayoangaza maendeleo ya Watanzania.

Aidha, Hemed alisema kupitia Muungano huo Tanzania ikishuhudia maendeleo makubwa na kuimarika kwa amani na utulivu nchini.

Pia, Hemed alisema serikali zote mbili zinatambua kazi kubwa zinazofanywa na Jeshi la Polisi na kuna kila sababu ya kuwapatia mazingira mazuri pamoja na vifaa na zana za kisasa za kufanyia kazi.

Alisema kuridhika kwake kuona fedha zilizotumika katika mradi hio zimetumika kwa mujibu wa thamani ya jengo hilo na kulipongeza Jeshi la Polisi Kamisheni ya Zanzibar kwa kusimamia matumizi mazuri ya fedha za Serikali na kuagiza kutunzwa kwa majengo hayo.

Aidha, alisema udhibiti mzuri wa matumizi ya fedha za serikali unatoa fursa ya kuendelea kujenga miradi mingine mipya ya kimaendeleo.

Hemed aliutaka uongozi wa Jeshi la Polisi, Kamisheni ya Zanzibar kusimami nidhamu kwa watendaji wake ili kujiepusha na mambo yote yanayoenda kinyume na maadili ya jeshi la polisi ikiwamo kujiepusha na rushwa, madawa ya kulevya, uhujumu wa uchumi, kutumia lugha mbaya kwa wananchi pamoja na ukosefu wa misingi ya utawala bora.

Naye Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alisema kwa kipindi cha miaka miwili, Kamisheni ya Polisi Zanzibar imepokea Sh. bilioni 5.79 kwa ajili ya kukamilisha miradi iliokuwa haijakamilika na ujenzi wa miradi mipya.

Alisema ujenzi wa majengo hayo mawili ya ofisi za Makamanda wa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja yamegharimu Sh. bilioni 3.3 na yamechukua miezi tisa hadi kukamilika.

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31-Machi-23 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Disemba-22 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,270 | 4,532 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 10,417 | 11,598 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43,973 | 43,956 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,775 | 6,091 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 74 | 37 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 98,773 | 100,998 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 127,159 | 125,843 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 20,361 | 20,880 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,286 | 2,455 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **313,089** | **317,389** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 55,677 | 69,845 |
| 18 | Amana za Wateja | 133,912 | 139,103 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,689 | 4,118 |
| 28 | Madeni | 93,051 | 92,809 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **286,329** | **305,875** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **26,759** | **11,514** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 139,306 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (114,427) | (97,171) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,138) | (17,288) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,018 | 3,018 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **26,759** | **11,514** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,945 | 1,945 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 8,256 | 7,265 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,400 | 6,412 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.55% | 3.63% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.18% | 5.49% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 70.45% | 65.49% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 40.61% | 39.65% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 47.85% | 48.36% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -9.26% | 1.23% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.35% | -2.32% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Marchi-23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31-Marchi-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Marchi-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Marchi-22 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,283 | 10,149 | 10,283 | 10,149 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,919) | (4,928) | (4,919) | (4,928) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,364** | **5,221** | **5,364** | **5,221** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | 311 | - | 311 |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,267** | **882** | **1,267** | **882** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 519 | 137 | 519 | 137 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 298 | 289 | 298 | 289 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 450 | 456 | 450 | 456 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,711)** | **(6,986)** | **(7,711)** | **(6,986)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,695) | (2,547) | (2,695) | (2,547) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,016) | (4,439) | (5,016) | (4,439) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,080)** | **(572)** | **(1,080)** | **(572)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (59) | (65) | (59) | (65) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,138)** | **(637)** | **(1,138)** | **(637)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,138)** | **(637)** | **(1,138)** | **(637)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 172 | 142 | 172 | 142 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.46) | (0.26) | (0.12) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.44% | -0.75% | -1.44% | -0.75% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -23.79% | -9.56% | -23.79% | -9.56% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 116.28% | 114.47% | 116.28% | 114.47% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.05% | 2.19% | 3.05% | 2.19% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Marchi-23 | Robo Mwaka iliyopita 31-Desemba-22 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,080) | (5,629) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 856 | 7,041 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,317) | 2,398 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (19,359) | 2,534 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (17) | (3,933) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (429) | 1,933 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 514 | (7,164) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (59) | (65) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(20,890)** | **(2,885)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (687) | (952) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(687)** | **(952)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 242 | 1,969 |
| | Mengineyo (bainisha) | 16,352 | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **16,594** | **1,969** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (4,984) | (1,869) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 123,219 | 125,087 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **118,235** | **123,219** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2023

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Non - Distributable Reserve | General Provision Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Current Year 2022** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the year** | **122,954** | **-** | **(114,427)** | **-** | **-** | **3,018** | **11,746** |
| Profit for the year | - | - | (1,138) | - | - | - | **(1,138)** |
| Issue of share | 16,352 | | | | | | |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | - | - | - | - | - | - | - |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | - | - | - | - | - |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | - | - | - |
| Others | - | - | - | - | - | - | - |
| **Balance as at the end of the current period** | **139,306** | **-** | **(115,565)** | **-** | **-** | **3,018** | **26,759** |
| **Previous Year 2022** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the year** | **122,954** | **-** | **(99,102)** | **2,163** | **-** | **989** | **27,004** |
| Profit for the year | - | - | (17,288) | - | - | - | **(17,288)** |
| Issue of share | - | - | - | - | - | - | - |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | 2,029 | **2,029** |
| Transactions with owners | - | - | - | - | - | - | - |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | 2,163 | (2,163) | - | - | - |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | - | - | - |
| Others | - | - | - | - | - | - | - |
| **Balance as at the end of the previous period** | **122,954** | **-** | **(114,427)** | **-** | **-** | **3,018** | **11,746** |

| | Name | Signature | Date |
|---|---|---|---|
| Managing Director | I. John | | 25-Apr-23 |
| Head of Finance | H. Kharbush | | 25-Apr-23 |
| Head of Internal Audit | J. Kilato | | 25-Apr-23 |

We, the under- named, non executive members of the board of directors, attest to the correctness of We declare that the above statements have been examined by us, and to the best of our knowledge prepared in conformance with the instructions and are true and correct.

| | Name | Signature | Date |
|---|---|---|---|
| 1 Director | P. Ishengoma | | 25-Apr-23 |
| 2 Director | Mr.R. Dave | | 25-Apr-23 |

217392301

# Wanaovunja sheria barabarani kukiona

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, amelitaka Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani kuwa wakali na kuwakamata wote wanaovunja sheria ili wasibaki salama.

Sagini aliyasema hayo wakati akizindua kituo cha polisi daraja A Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe. Alisema wanapaswa kuongeza ukali katika kusimamia sheria ili kupunguza ajali.

"kwenye hili niwapongeze wana Njombe, Iringa na Mbeya, mmekuwa mkifanya juhudi sana kudhibiti matukio ya ajali za barabarani ingawa ajali hizo hutokea ombi langu kwenu Kamishna Sabas ongezeni ukali maana sheria za usalama barabarani hazisimamiwi ni sawa na kazi bure, najua mnazo changamoto mnakamata baadhi ya mabasi mnapigiwa simu nyingi kweli, lakini naamini hamjawahi kupata simu ya mh Hamadi Masauni wala simu yangu mimi, kwa hiyo endeleeni kuwa imara, simamieni sheria bila ya kuonea mtu, lakini msimpendelee mtu," alisema.

"Niliwahi kusema wakati fulani inaumiza sana kila mara mnamsikia Rais wetu kutuma salamu za rambirambi kwa wakuu wa mikoa kutokana na ajali za ovyo ovyo zinazotokana na uendeshaji hatarishi kwa hiyo nitumie jukwaa hili kuagiza tena trafiki polisi ambapo mimi ni wenyekiti wao wa usalama barabarani taifa waendelee kuwa wakali, kwa hiyo mkazo kutoka kwangu na kwa waziri wangu kukamia wote wanaovunja sheria wasibaki salama," alisema Sagini.

Pia aliagiza Jeshi la Polisi kuendelea kuwajibika ipasavyo kwa kuimarisha kamisheni ya polisi jamii inayosisitiza wananchi kuchukia uhalifu na wahalifu na kuwa sehemu muhimu ya kusaidia jeshi hilo kutekeleza majukumu ya kupambana na uhalifu ya wananchi pamoja na kulinda mali zao.

Awali akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna wa Polisi Liberatus Sabas, alisema Julai 2022 hadi Machi 2023 makosa ya jinai yaliyotolewa taarifa 40,763 ikilinganishwa na mwaka 2021/22 jumla ya makosa 39,179 hivyo kuwa na ongezeko la makosa 1,584.

"Ongezeko la makosa haya makubwa ni kutokana na makosa ya ubakaji, ulawiti na mauaji na vyanzo vya makosa ya mauaji ni pamoja na kujichukulia sheria mkononi, wivu wa mapenzi, imani za kishirikina pia ndugu kugombea mirathi," alisema.

Aidha, vitendo vya ulawiti na ubaji vinatokana na mmomonyoko wa maadili unaotokana na ulegevu wa kushindwa kujizuia dhidi ya tamaa ya mapenzi, ukosefu wa malezi bora na imani za kishirikina.

Makosa ya usalama barabrani kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2023, jumla ya matukio ni 1,153 ikilinganishwa na makosa 1,594 mwaka 2022, kumekuwapo na pungufu ya matukio 441 sawa na asilimia 27.7.

"Kupungua kwa matukio haya ni kutokana na usimamizi wa sheria, kufanyika kwa operesheni maalumu, doria, misako nchi nzima na elimu ya usalama barabarani imeendelea kutolewa kwa makundi yote yanayotumia barabara ni mkakati maalumu wa mandeleo," alisema Sabas.

Kamanda wa polisi mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho alisema kimegharimu Sh. milioni 900.

## Temeke yaongoza vifo vya Malaria

**Na Joseph Mwendapole**

WILAYA ya Temeke jijini Dar es Salaam inaongoza kwa vifo vingi vya malaria kwa kuwa na vifo 17 mwaka 2022 ikifuatiwa na Wilaya ya Ilala iliyokuwa na vifo 13 kwa mwaka huo.

Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa Malaria, Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ford Chisongela, wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuelekea siku ya malaria duniani ambayo kimataifa inafikia kilele leo.

Alisema inayofuata ni Wilaya ya Konondoni iliyokuwa na vifo 12, Wilaya ya Ubungo vifo viwili na Wilaya ya Kigamboni haikuwa na vifo kwa mwaka huo na ndiyo inayoongoza kwa kuwa na maambukizi kidogo kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema kwa kiwango cha maambukizi, Wilaya ya Ilala inaongoza kwa kuwa na asilimia 1.7 ya maambukizi wakati wilaya inayofuata ya Ubungo yenye asilimia 0.7, Kinondoni asilimia 0.7, Temeke asilimia 0.6 na Kigamboni asilimia 0.5.

Alisema kwa Mkoa wa Dar es Salaam maambukizi ya malaria yameendelea kushuka na hadi mwaka juzi maambukizi kimkoa yalikuwa chini ya asilimia 0.7.

Alisema takwimu hizo zilipatikana baada ya utafiti uliofanywa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwapima wanafunzi wa shule za msingi na kwa miaka mitano wagonjwa wa nje wanaotibiwa ugonjwa huo wamepungua.

Alisema kwa mwaka 2018-2022 maambukizi yamepungua kwa asilimia 40 kwa wagonjwa wanaofika hospitalini kutibiwa na kuondoka wakati kwa wanaolazwa umepungua kwa asilimia 25.

Alisema vifo kwa wagonjwa wanaolazwa na wanaokwenda kutibiwa na kuondoka kwenye hospitali mbalimbali za mkoa huo vimepungua kwa asilimia 25 huku Temeke ikiwa na vifo vingi zaidi.

Alisema ili kukabiliana na ugonjwa huo, mkoa umekuwa ukifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha watu wanaokutwa na maambukizi ya ugonjwa huo wanapata matibabu sahihi kusaidia kupunguza mzunguko wa malaria.

Dk. Ford alitaja mkakati mwingine kuwa ni kuhakikisha kila mjamzito anapata chandarua anapokwenda kliniki kwa mara ya kwanza.

Aidha, alisema mkakati mwingine ni kugawa vyandarua kwa wanafunzi wa shule za msingi kwa mwaka jana pekee walifanikiwa kugawa kwa wanafunzi 17,000.

Alisema mkakati mwingine ni kunyunyuzia dawa kwenye vyanzo vya mazalia ya mbu kwenye kata zote 102 za Mkoa wa Dar es Salaam mara moja kila mwezi na umesaidia kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo.


BancABC part of atlasmara

**AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED**

**MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES**

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

**AGENCY BANKING FEE**

| | |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Bill payment | Free |

**Withdrawal Fees**

| Transaction tiers | BancABC Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 0-999 | N/A | - | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |

217392302

HABARI MICHEZO

# RUVU SHOOTING SASA INAHITAJI MAOMBI KUBAKI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Maafande wa JKT Tanzania wakipanda Ligi Kuu, hali imeendelea kuwa mbaya kwa ndugu zao Ruvu Shooting baada ya Jumamosi kupoteza tena mechi yake kwa mabao 3-1 dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, ikizidi kudidimia kwenye shimo la kushuka daraja kwenda kwenye Ligi ya Championship.

Kipigo hicho kimeifanya kuendelea kukamata mkia ikiwa na pointi 20 kutokana na mechi 27 ilizocheza mpaka sasa, ikisalia na mechi tatu tu za kumaliza msimu.

**Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbwana Makata, amesema watajitahidi kila njia kupata pointi tisa zilizobaki kwenye mechi tatu ili waangalie wataangukia wapi, huku wao pia wakiwa hawana ukakika na wapo tayari kwa chochote kitakachotokea.**

"Tumejitahidi sana kadri ya uwezo wetu, haya yanayotokea ni kwa sababu mwanzo haukuwa mzuri, tungekuwa na mwanzo mzuri tusingefika hapa, kwenye mechi zilizosalia tutapambana na tutakubaliana na chochote kitakachotokea," alisema Makata.

Ruvu imeshinda mechi tano tu mpaka sasa kwenye Ligi Kuu msimu huu, ikiwa ni moja kati ya timu zilizoshinda mechi chache pamoja na Polisi Tanzania, huku ikipoteza mechi 17 ambazo ni nyingi kuliko timu yoyote kwenye ligi hiyo.

Pamoja na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Ushirikia mjini Moshi, bado Polisi Tanzania haipo sehemu salama kwenye ligi hiyo kwani inashika nafasi ya 15 ikiwa na pointi 22, mbili juu ya wanaoshika mkia Ruvu Shooting, nayo ikiwa imebakisha mechi tatu ili kujua hatma yake kama itashuka, kucheza 'play off' au kujiokoa na vyote.

Timu ya KMC, pamoja na kumchukua kocha Jamhuri Kihwelo 'Julio', baada ya kumfurusha Thierry Hitimana, bado haikuwa dawa baada ya kutwangwa bao 1-0 Jumamosi iliyopita dhidi ya Dodoma Jiji katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

KMC nayo iko eneo la hatari ikiwa na pointi zake 26, nafasi ya 14, ikibakisha mechi tatu nayo kumaliza mechi zake 30 za msimu huu.



Mwenyekiti wa Ndanda FC, Geofrey Lukanga (kushoto), akiwa na Katibu Mkuu wa timu hiyo, Selemani Kachele, wakati wakizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Mtwara kuhusu kuvunja kambi ya timu hiyo baada ya kukosa fedha za kuisafirisha kwenda jijini Mwanza kwa mchezo wa Ligi ya Championship dhidi ya Capco FC unaotarajiwa upigwe leo katika Uwanja wa Nyamagana. **PICHA: BARAKA JAMALI**

## Simba Queens na Hesabu za ubingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, ameanza kuzipigia hesabu mechi nne za kutetea taji lao la ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania huku akiiombea JKT Queens kutoka sare ama kupoteza mchezo mmoja.

Simba Queens ambayo ina pointi 33 moja nyuma ya vinara wa ligi hiyo, JKT Queens, imebakiza mechi dhidi ya Aman Queens Aprili 24 na Mei 5 watawakaribisha Alliance Girls na kisha kwenda ugenini kucheza dhidi ya Baobab Queens Mei 9 na Mei 17, mwaka wakihitimisha msimu kwa kucheza dhidi ya Ceasiaa Queens.

Akizungumza na Nipashe jana, Lukula alisema msimu ligi imekuwa ngumu na kwamba kutetea ubingwa wao lazima kushinda mechi zote nne zilizosalia bila kuangalia matokeo ya timu nyingine.

Alisema kila mechi kwao ni muhimu kukusanya pointi zote tatu na kila na atafanya mabadiliko ya kikosi kila mechi kulingana na wachezaji wake wanavyoonyesha uwezo mazoezini.

"Hakuna mechi iliyokuwa rahisi kila mchezaji natambua umuhimu wake, nitakuwa na mabadiliko ya kikosi kulingana na mpinzani tunayekutana naye.

"Mabadiliko yanaendelea kuwapo ndani ya kikosi changu katika hii michezo iliyosalia kulingana na uwezo na viwango vitakavyoonyeshwa mazoezini na wachezaji wangu, nahitaji kila mtu apate nafasi ya kucheza," alisema.

Aliongeza: "Tunatakiwa kushinda hizi mechi nne zilizosalia hatuhitaji kumfuatilia mpinzani wetu anayeongoza ligi, kwa sababu ukiangalia tumepishana naye pointi moja, akiteleza mchezo mmoja na sisi tukishinda tunamshusha na kuongoza msimamo," alisema Lukula.

Kwa upande wa JKT Queens, imebakiza mechi dhidi ya The Tiger Queens, Fountain Gate, Yanga Princess na Mkwawa Queens.

# Ndanda FC yashindwa kuifuata Capco Mwanza

**Na Baraka Jamali,** MTWARA

UONGOZI wa Klabu ya Ndanda yenye masikani yake mkoani Mtwara, imeshindwa kuisafirisha timu hiyo kuipeleka jijini Mwanza, walipopaswa kucheza mchezo namba 223 wa Ligi ya Championship dhidi ya Copco fc ambao ulipagwa kupigwa Uwanja Nyamagana leo Jumanne, kutokana na kukosa fedha.

Akizungumza na vyombo vya habari mkoani Mtwara jana, Mwenyekiti wa Ndanda FC, Geofrey Lukanga, alisema wameshindwa kuisafirisha timu hiyo kwenda kucheza mchezo huo kutokana na kukosa fedha ya mafuta na mahitaji mengine ya wachezaji hali iliyosababisha wachezaji kuruhusiwa kuondoka kambini.

"Tulikuwa na mchezo kesho [leo] dhidi ya Copco katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, lakini kutokana na kukosa fedha za kuisafirisha timu, tumeamua kuwaruhusu wachezaji waondoke kambini na kama tutapata fedha basi tutawataarifu ili kuwahi kucheza mchezo wa Mara [Aprili 24, mwaka huu], lakini kwa Sasa tumeshindwa kabisa kusafirisha timu," alisema Mwenyekiti huyo.

Aliendelea kueleza: Tumewatafuta wadau akiwamo mlezi wetu Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, lakini jitihata zetu zimegonga mwamba, ili tuweze kufanikisha michezo yetu mitatu ya nje tunahitaji kuwa na milioni 25, lakini mpaka sasa tumekwama ingawa tunajua ni jambo linaloumiza, lakini kwa sasa hatuna cha kufanya zaidi ya kuifunga kambi ya timu yetu".

Aidha, kwa upande wa Mkurugenzi wa timu hiyo na Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mtwara, Athumani Kambi, aliwaeleza waandishi wa habari kwamba alikuwa na uwezo wa kuipatia timu hiyo Sh. milioni 1.5 au mbili, lakini haikutosha kuisafirisha timu hiyo na kwamba imetumika kuwapa wachezaji hao nauli za kurejea kwao kutokana na hali hiyo mbaya.

Alisema: "Kama tukipata fedha leo tutawaomba TFF waweze kuipeleka mechi hiyo Ijumaa ili tucheze kwa sababu nia tunayo, lakini hatuna fedha kwa sasa na wadau wameonesha kutotuunga mkono kwa wakati huu, lakini tuliwafuata ili watusaidie kuisafirisha timu, sipendezwi na uamuzi huu, lakini timu ilibaki kwangu peke yangu ila siwezi kuiendesha kwa sasa".

Ndanda fc msimu huu ina alama 15 ikiwa nafasi ya 15 kati ya timu 16 zinazo shiriki ligi hiyo na imesaliwa na michezo minnne dhidi ya Copco ya Mwanza, Biashara ya Mara, Pan African ya Dar es salaam na dhidi ya Transit Camp itakayopigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEYMAR KUPIGWA BEI

KLABU ya Paris St-Germain inafikiria kumuuza Neymar, 31, msimu huu wa majira ya joto - huku Chelsea na angalau klabu nyingine moja ya Ligi Kuu England ikitafakari kumnunua mshambuliaji huyo. ***(Mirror)***

### MESSI KURUDI BARCA

MSHAMBULIAJI wa PSG, Lionel Messi, 35, anataka kurejea Barcelona, lakini klabu hiyo ya Hispania inahitaji kuongeza pauni milioni 88 kupitia mauzo ya wachezaji na kuamsha 'kichocheo kingine cha kiuchumi' ili kumsajili tena. ***(Mail)***

### KANE ALENGWA BAYERN

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, 29, yuko kwenye orodha ya wanaolengwa na Bayern Munich msimu huu wa joto, ingawa nahodha huyo wa England anaaminika kusita kuondoka Ligi Kuu England. ***(Bild)***

### KOULIBALY ATAKIWA JUVE

JUVENTUS inapanga kumnunua mlinzi wa Senegal, Kalidou Koulibaly, 31, ambaye hajafurahia hali yake baada ya msimu mmoja tu akiwa Chelsea. ***(Gazzetta dello Sport)***

### GVARDIOL BAS LIVER

LIVERPOOL imepunguza nia ya kumnunua mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol, 21, kwani wanaamini kwamba thamani ya pauni milioni 80 inayotakiwa na Red Bull Leipzig kwa mchezaji huyo ni kubwa mno. ***(Football Insider)***

### HICKEY ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inapanga kumnunua beki wa pembeni wa Brentford kutoka Scotland, Aaron Hickey, 20, ambaye thamani yake ni pauni milioni 30. ***(Sun)***

### ENRIQUE HATAKIWI TENA

KOCHA wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, hayupo tena kwenye kinyang'anyiro cha kuwa kocha mpya wa Chelsea. ***(Fabrizio Romano)***

### POCHETTINO AWINDWA

WACHEZAJI wa Chelsea wamefurahishwa na uwezekano wa kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino kuwa kocha wao mpya. ***(Telegraph)***

### MUSAH AWANIWA EPL

ARSENAL, Chelsea na Liverpool zimeonesha nia ya kutaka kumnunua beki wa Valencia, Yunus Musah, 20, kutoka Marekani. ***(90Min)***

### CHELSEA YAMZUIA COLWILL

CHELSEA haina nia ya kumuuza mlinzi wa England aliye chini ya umri wa miaka 21, Levi Colwill, 20, msimu huu wa majira joto licha ya Liverpool, Tottenham Hotspur na Manchester City kumtaka. ***(Football Insider)***

### FOWLER AUTAKA UKOHA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool na England, Robbie Fowler, anafikiria kutuma ombi la kuajiriwa kama kocha katika klabu ya Ligi ya Daraja la Pili ya Tranmere Rovers. ***(Sun)***

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA



# 'SALAH HATHAMINIWI'

**LIVERPOOL,** England

UFUNGAJI wa mabao wa Mohamed Salah hauthaminiwi na wale waliopo nje ya Liverpool, anaamini mchezaji mwenzake, Virgil van Dijk.

**Salah alifunga bao lake la 183 kwa Liverpool wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Nottingham Forest Jumamosi, baada ya Neco Williams na Morgan Gibbs-White kufunga wakisawazisha mawili ya Diogo Jota.**

Bao la ushindi la raia huyo wa Misri lilimfanya kufikia idadi ya mabao ya Robbie Fowler kwa Liverpool katika mechi 71, na kumfanya ajiweke nafasi ya sita kwenye orodha ya wafungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo.

Salah, amefunga mabao 27 katika mashindano yote msimu huu wakati Liverpool ikiwa haina matokeo ya kuridhisha, na sasa anaiwania rekodi ya mabao 186 aliyofunga Steven Gerrard.

Alipoulizwa kuhusu ufungaji wa mabao wa Salah baada ya ushindi wa Jumamosi, Van Dijk alisema fowadi huyo anadharauliwa na wale ambao si mashabiki wa 'Wekundu' hao.

"Wachezaji wengi hapa wamechangia kushinda mataji makubwa. Mo hakika ataonekana kama gwiji. Ni mchezaji muhimu sana," alisema Van Dijk akiwaambia waandishi wa habari.

"Baadaye, nadhani mambo ambayo amefanya yatathaminiwa zaidi na ulimwengu wa nje.

> ●●● Baadaye nadhani mambo ambayo amefanya yatathaminiwa zaidi na ulimwengu wa nje...

"Kwetu sisi, tunathamini kila kitu anachofanya siku baada ya siku. Tunaona kazi ngumu anayoweka. Ni lazima aendelee nayo."

Akiwa amefunga pia katika sare ya 2-2 dhidi ya Arsenal kabla ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa 6-1 dhidi ya Leeds United, Salah sasa amefunga katika mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu Oktoba 2021 (wakati alipofunga kwenye mechi saba mfululizo).

Liverpool imebaki na pointi tisa kutoka kwenye nafasi nne za juu licha ya kushinda mechi mfululizo, na Van Dijk amesema msimu wa timu hiyo kuwa chini ya kiwango umewafungua macho.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 560,

MECHI KALI

GIRONA
VERSUS
REAL MADRID

1 | 5.15
X | 3.82
2 | 1.58

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN UNITED KUIZUIA CITY KUTWAA MA3



**LONDON,** England

ERIK ten Hag amesema Manchester United "itatoa kila kitu" kuwazuia Manchester City kuwaiga kwa kutwaa mataji matatu msimu huu kama ilivyokuwa kwa 'Mashetani Wekundu' hao mwaka 1999, baada ya kutinga fainali ya Kombe la FA, Jumapili.

City wapo kwenye kinyang'anyiro cha mataji matatu, Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA msimu huu, lakini watalazimika kuwafunga majirani zao United kwenye fainali ya Kombe la FA Juni 3, mwaka huu ikiwa wanataka kushinda mataji yote matatu.


Na Ten Hag, ambaye alishuhudia United ikishinda mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Brighton Jumapili, amewahakikishia mashabiki kuwa watafanya kila kitu kuwazuia City kutwaa kombe hilo na hivyo kuhifadhi rekodi ya United kama timu pekee ya England kushinda mataji matatu kwa msimu mmoja.

"Tutatoa kila kitu na ninaposema kila kitu, maana yake ni zaidi ya asilimia 100, mashabiki wanaweza kutegemea hilo," alisema Ten Hag.

"Tunataka kufanya hivyo dhidi ya City, tunataka kuwapa mashabiki hilo. "Lazima tucheze mchezo kamili, ulikuwa mchezo mzuri tuliocheza msimu huu, lazima turudi tena, tunajua hilo.

"Lakini kwanza tunapaswa kuzingatia matukio tofauti kwa sababu lazima tuwe katika nafasi nne za juu."

Baada ya kuishinda Brighton pale Wembley, Ten Hag pia alisifu kiwango cha timu yake, haswa baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Europa na Sevilla, Alhamisi iliyopita.



## Xavi: Kazi bado ipo Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona Xavi amezungumzia umuhimu wa ushindi wa Barcelona dhidi ya Atletico Madrid huku viongozi hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakirejea katika njia yao ya ushindi Jumapili.

Ferran Torres alifunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 kwenye Uwanja wa Camp Nou, na kuhitimisha msururu wa kutofunga mabao uliojumuisha sare tasa mfululizo kwenye ligi.

Ushindi huo pia umeongeza uongozi wa Barca kileleni mwa msimamo wa LaLiga hadi pointi 11 juu ya wapinzani wao, Real Madrid.

Zikiwa zimebaki mechi nane ligi hiyo kufikia ukingoni msimu huu, Barca wanakaribia kutwaa ubingwa, lakini Xavi aliweka wazi kuwa bado kuna kazi ya kufanya.

"Hakuna kilichofanyika bado, ingawa inafurahisha," alisema. "Hapa, hakuna mtu anayejisikia kama bingwa, na ikiwa mtu atafanya hivyo, tutawaambia kuwa hakuna kitu ambacho kimefanywa.

Ushindi wa Barca haukuwa mzuri kama inavyopaswa kuwa, huku Robert Lewandowski na Raphinha wakiwa miongoni mwa waliopoteza nafasi za wazi za kufunga, jambo ambalo Xavi alilaumu.

"Nina hisia ya kupoteza nafasi za kufanya matokeo kuwa 2-0; walikuwa wazi sana," alisema. "Rapha, Robert, na Gavi walikosa nafasi za wazi eneo la penalti.

,305,280

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/04/23 | 21:30 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.20 | 3.15 | 3.15 |
| 02. 25/04/23 | 21:45 | Lincoln vs Burton | 2.21 | 3.37 | 3.16 |
| 03. 25/04/23 | 22:00 | Leeds vs Leicester | 2.20 | 3.49 | 3.09 |
| 04. 26/04/23 | 01:30 | CA Tigre vs Huracan | 2.36 | 3.01 | 2.91 |
| 05. 26/04/23 | 13:00 | Gangwon vs FC Seoul | 2.53 | 2.93 | 2.67 |
| 06. 26/04/23 | 13:00 | Gwangju vs Jeju Utd | 2.72 | 3.03 | 2.42 |
| 07. 26/04/23 | 13:30 | Suwon City vs Daegu | 2.48 | 3.18 | 2.54 |
| 08. 26/04/23 | 18:30 | Hradec Kralove vs Slovan Liberec | 2.27 | 3.05 | 3.21 |
| 09. 26/04/23 | 21:30 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.31 | 3.26 | 2.89 |
| 10. 26/04/23 | 22:00 | Sheffield Utd vs West Bromwich | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 11. 27/04/23 | 21:45 | Southampton vs Bournemouth | 2.26 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 27/04/23 | 22:00 | Rotherham vs Cardiff | 2.80 | 2.80 | 2.65 |
| 13. 27/04/23 | 22:15 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.59 | 3.27 | 2.51 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 25/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5031 | Pohang Steelers vs Suwon Samsung | 1.83 | 3.23 | 3.95 |
| 13:30 | 5117 | Incheon Utd vs Ulsan Hyundai | 3.29 | 3.19 | 2.03 |
| 14:35 | 5104 | Meizhou Kejia vs Wuhan Three Towns FC | 4.51 | 3.49 | 1.66 |
| 15:00 | 1159 | Sioni Bolnisi vs FC Spaeri | 2.05 | 3.37 | 3.16 |
| 15:00 | 1838 | Torpedo Kutaisi vs Saburtalo Tbilisi | 2.16 | 3.17 | 3.11 |
| 15:00 | 2136 | Bristol City U23 vs Wigan U23 | 2.17 | 3.70 | 2.45 |
| 15:00 | 4070 | Legetafo Legedadi vs Hadiya Hosahina FC | 6.01 | 3.73 | 1.50 |
| 15:00 | 4420 | Lernayin Artsakh vs Artsakh | 2.74 | 2.95 | 2.52 |
| 15:00 | 4828 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs Loko Tbilisi | 2.13 | 3.22 | 3.12 |
| 16:00 | 3515 | Mamelodi Sundowns vs Richards Bay FC | 1.35 | 4.40 | 8.17 |
| 17:00 | 2604 | FC Famalicao U23 vs Estoril Praia U23 | 2.35 | 3.53 | 2.56 |
| 17:00 | 3305 | FC Vizela U23 vs Benfica U23 | 2.57 | 3.53 | 2.34 |
| 17:00 | 4761 | Estrela Amadora U23 vs SP. Braga U23 | 2.43 | 3.15 | 2.43 |
| 17:30 | 1185 | NK Bistrica vs Maribor | 14.45 | 5.78 | 1.17 |
| 17:30 | 1548 | AL Tadamon vs AL Nasr | 3.49 | 3.80 | 1.79 |
| 18:00 | 4979 | Adama City FC vs Sidama Bunna SC | 2.03 | 3.05 | 3.57 |
| 18:00 | 5709 | FC Riga vs FS Metta/Lu | 1.13 | 6.63 | 15.55 |
| 18:30 | 2719 | Teplice vs Mlada Boleslav | 2.96 | 3.43 | 2.22 |
| 18:30 | 5641 | Pardubice vs Slovacko | 2.96 | 3.28 | 2.29 |
| 18:45 | 2142 | Sitra Club vs AL Badii | 1.35 | 4.35 | 7.87 |
| 18:45 | 5221 | Muharraq SC vs Manama Club | 2.04 | 3.06 | 3.53 |
| 18:55 | 3565 | Alshoulla vs AL Arabi (SA) | 3.70 | 3.08 | 1.94 |
| 19:00 | 2369 | Dinamo Tbilisi vs Dila Gori | 1.68 | 3.25 | 4.20 |
| 19:00 | 3976 | HNK Sibenik vs Slaven Belupo | 2.40 | 3.08 | 2.72 |
| 19:30 | 2277 | Vorwarts Steyr vs Amstetten | 2.54 | 3.15 | 2.56 |
| 19:30 | 2934 | Al Orubah vs Najran SC | 2.03 | 3.07 | 3.43 |
| 20:00 | 1507 | Duisburg vs SV Elversberg | 4.23 | 3.86 | 1.71 |
| 20:00 | 3676 | Dinamo Bucuresti vs FC Politehnica Iasi | 2.41 | 2.93 | 2.82 |
| 20:00 | 4913 | Vasteras SK vs Orebro SK | 1.86 | 3.53 | 4.01 |
| 20:00 | 5249 | HB Torshavn vs Vikingur Gota | 1.77 | 3.55 | 3.80 |
| 20:00 | 5346 | Al Jahra vs AL Sahel | 2.11 | 3.25 | 3.04 |
| 20:30 | 3234 | Banik Ostrava vs Slavia Prague | 4.97 | 4.18 | 1.56 |
| 20:30 | 4305 | Saint Brieuc vs Nancy | 2.74 | 3.00 | 2.59 |
| 20:30 | 4463 | Cadiz CF vs Osasuna | 2.11 | 3.05 | 3.46 |
| 20:30 | 4888 | Girona vs Real Madrid | 5.15 | 3.82 | 1.58 |
| 20:40 | 3493 | AL Khlood vs Hajer Club | 2.02 | 2.85 | 3.35 |
| 21:30 | 3640 | Grasshoppers vs BSC Young Boys | 5.16 | 4.32 | 1.52 |
| 21:30 | 3650 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.22 | 3.10 | 3.15 |
| 21:30 | 4219 | Sporting Braga vs Nacional Madeira | 1.15 | 6.42 | 13.46 |
| 21:45 | 1099 | Boreham Wood vs Gateshead | 1.83 | 3.42 | 4.05 |
| 21:45 | 2220 | Woking vs Halifax | 1.61 | 3.57 | 5.46 |
| 21:45 | 2493 | Aston Villa vs Fulham | 1.72 | 3.70 | 4.20 |
| 21:45 | 2862 | Plymouth vs Bristol Rovers | 1.42 | 4.45 | 6.68 |
| 21:45 | 3032 | Bolton vs Accrington | 1.49 | 4.12 | 6.03 |
| 21:45 | 3414 | Oxford Utd vs Cheltenham | 1.66 | 3.73 | 4.74 |
| 21:45 | 3488 | Lincoln vs Burton | 2.03 | 3.38 | 3.43 |
| 21:45 | 4839 | Barnsley vs Ipswich | 3.44 | 3.34 | 2.04 |
| 22:00 | 4050 | Leeds vs Leicester | 2.16 | 3.40 | 3.00 |
| 22:00 | 5316 | Blackburn vs Burnley | 3.40 | 3.20 | 2.07 |
| 23:00 | 2704 | Betis vs Real Sociedad | 3.05 | 3.20 | 2.23 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# YANGA KUMPA IBRAHIM BACCA MIAKA MIWILI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema uko katika hatua za mwisho za kumwongezea mkataba wa miaka miwili beki wao, Abdallah Ibrahim 'Bacca'.

Bacca (pichani) mkataba wake unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu na amekuwa na kiwango kizuri ndani ya kikosi cha Yanga ambapo ameingia kwenye vita vya kugombea namba katika kikosi cha kwanza kinachonolewa na Kocha Nasreddine Nabi.

**Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alisema Bacca ni beki mzuri na ameonyesha kiwango kizuri na kuwa miongoni mwa wachezaji walioitwa kikosi cha Timu ya Taifa, Taifa Satars na kuleta ushindani mkubwa wa namba.**

"Ukitaka kupata matokeo mazuri lazima tufanye usajili mzuri pia kuwa na benchi la ufundi zuri, viongozi tunafanya kazi kubwa sana katika usajili kwa sababu unatakiwa kusajili zaidi ya wachezaji watatu wanaocheza nafasi moja kama ilivyo kwa hapa Yanga.

"Tumeanza kufanya naye mazungumzo juu ya mkataba mpya na safari hii tunauboresha kwa kumpa maslahi mazuri, ninaimani tumefanya usajili mzuri sana kuanzia Bacca na wachezaji wengine waliopo hapa Yanga," alisema Hersi.

Alisema jambo kubwa ambalo watamfanyia wiki ijayo beki huyo ni kumuongezea mkataba mwingine ambao utakuwa na maslahi mazuri kulingana na kile anachokionyesha uwanjani.

Hersi alisema uongozi uko makini katika suala la kufanya usajili kwa kuangalia nini timu inahitaji hasa wanapohitaji kusajili mchezaji ambaye atakuja kuisaidia timu.

"Tumemkosa Mshery [Abdultwalib], lakini tukaenda kumsajili Metacha [Mnata] na tumeona mechi ya marudiano dhidi ya TP Mazembe alivyodaka vizuri na kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo," alisema Hersi.




## Simba waitaka rekodi ya 2003

INATOKA UK. 24

chao na anaimani kubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano nchini Morocco.

Alisema wanaitaka nusu fainali na kufikia rekodi ya mwaka 2003 ya kumuondoa bingwa mtetezi katika ardhi ya nyumbani kwake, na ili kutimiza malengo hayo mchezo wa marudiano wataingia tofauti kabisa kwa kuwa kila mchezaji ataingia katika mechi hiyo akiwa na moyo wa Simba.

Alisema kuhakikisha wanakuwa imara kuanzia nje na ndani ya uwanja, tayari Mratibu wa Simba, Abbas Ally, ameshatangulia nchini Morocco kuweka mazingira mazuri ya kufikia timu hiyo.

Kwa upande wa benchi la ufundi la klabu hiyo, Kocha Msaidizi, Juma Mgunda, aliliambia Nipashe kuwa lengo lao ni kwenda kufanya vizuri katika mchezo huo ili waingie hatua ya nusu fainali.

"Sasa hivi tunaelekeza nguvu na akili kwenye mchezo wetu wa marudiano, tutakwenda tukiwa na tahadhari kwani tunafahamu ugumu wa mchezo huo," alisema Mgunda.

## *Yanga yautaka ubingwa*

INATOKA UKURASA 24

pamoja na uongozi na kwamba anatarajia kuendeleza kasi hiyo ya mabao katika mchezo wa marudiano Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Mchezo wa marudiano ambao tutaucheza nyumbani, nitaendeleza ushindani kwani lengo ni kuingia hatua ya nusu fainali," alisema mshambuliaji huyo.

Alisema anashukuru kuona timu yao imevunja mwiko kwa kuifunga Rivers United nyumbani kwao baada ya msimu uliopita Wanigeria hao kuifunga Yanga bao 1-0 nyumbani na ugenini kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Awali malengo ya Yanga yalikuwa kutinga hatua ya makundi, lakini sasa yamebadilika na kuwa kutwaa taji hilo la Kombe la Shirikisho.

# Michezo

Jumanne Aprili 25, 2023

Nipashe




'Salah hathaminiwi' UKURASA 21

NUSU ILEEE...




Wachezaji wa Yanga, kutoka kushoto Kennedy Musonda, Khalid Aucho, Fiston Mayele na Tuisila Kisinda, wakishangilia baada ya timu yao kuichapa Rivers United mabao 2-0 kwenye mechi ya robo fainali mkondo wa kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Godswill Akpabio nchini Nigeria juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga sasa yautaka ubingwa wa Shirikisho*

## ●●● Yabadili gia ya malengo angani, Mayele asema amelipa kisasi, aahidi makubwa zaidi...

**Adam Fungamwango na**

**Shufaa Lyimo**

USHINDI wa mabao 2-0 dhidi ya Rivers United ilioupata kwenye Uwanja wa Godswill Akpabio nchini Nigeria juzi, umeipa jeuri Yanga, ikisema kwa sasa inauhitaji ubingwa huo wa Kombe la Shirikisho barani Afrika.

**Rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said amesema, awali hawakuwa na matarajio hayo, lakini kadri muda unavyozidi kwenda na wao kupata mafanikio wanaona inawezekana kabisa kutwaa kombe hilo na kuipa sifa nchi ya Tanzania.**

Akizungumza baada ya kumalizika mechi hiyo nchini Nigeria, Hersi alisema lengo la klabu kubwa kama Yanga ni kutwaa mataji na inapofika kipindi njia inaonekana basi ni wakati wa kuifuata.

Yanga ni timu kubwa na kongwe, tangu tuko wadogo tumeikuta lengo lake ni kutafuta mataji, sishangai nikiona malengo yetu ya kutafuta ubingwa wa Afrika kwenye michuano hii yanaanza kuonekana.

Awali, tulianza michuano hii taratibu, hakuna aliyetutilia maanani, tukaingia hatua ya makundi na tukaweza kuchukua nafasi ya kwanza kwenye kundi letu jambo ambalo halijawahi kutokea kwa klabu hii, lakini tukaingia robo fainali na leo tumemaliza dakika 90 za kwanza, tukivuka huko, chochote kinaweza kutokea.

"Siku zote unapoingia kwenye mashindano malengo makubwa ya mwisho ni kuchukua kombe japo kuna malengo ya mwanzo, na kwa nini isiwe Yanga kutwaa kombe hili la Shirikisho Afrika? Itakuwa ni furaha kwa wanachama, mashabiki wetu, Watanzania na furaha kwa taifa zima," alisema Rais wa klabu hiyo.

Akizungumzia ushindi ambao timu yake iliupata, alisema umekuwa na umuhimu mkubwa kwani tayari wameshaweka mguu mmoja kwenye hatua ya nusu fainali.

"Ulikuwa ni ushindi muhimu kwetu, tunaweza kusema tumeweka mguu mmoja kwenye nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, safari bado ni ndefu, tunahitaji kwenda kucheza dakika zingine 90 nyumbani, tunahitaji kucheza kwa heshima kabisa na tahadhari kubwa, Rivers United siyo timu ndogo, imekuwa na matokeo mazuri, kitu kinachotakiwa ni kuimaliza mechi Dar es Salaam, kulinda ushindi huu tulioupata ugenini na ikiwezekana kushinda kabisa," alisema.

Naye Afisa Habari wa klabu hiyo Ali Kamwe alifichua mbinu za Kocha Mkuu Mtunisia Nasreddine Nabi kwenye mechi hiyo hadi kuibuka na ushindi.

Naye mfungaji wa mabao yote mawili katika mchezo huo, Fiston Mayele, alisema ametimiza ahadi yake ya kuifunga Rivers United katika mchezo huo wa robo fainali.

Mayele alisema: "Kabla ya mchezo huu nilisema lazima nilipe kisasi, hatimaye ndoto zangu zimetimia ni mchezo ambao nilikuwa ninausubiri kwa hamu".

Alisema siri ya mafanikio yao imetokana na ushirikiano uliopo baina ya wachezaji kwa wachezaji, benchi la ufundi

INAENDELEA UKURASA 23

## Simba waitaka rekodi ya 2003

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuifunga timu ya Wydad Casablanca bao 1-0 katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi iliyopita, benchi la ufundi la Simba limesema linajipanga kwenda kufanya tena kweli nchini Morocco huku uongozi wa klabu hiyo ukisema unaitaka rekodi yao ya mwaka 2003.

Katika michuano hiyo, mwaka 2003 ikiwa ni miaka 20 iliyopita, Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya mabingwa watetezi wa wakati huo, Zamalek ya Misri, na katika mechi ya marudiano ugenini, Wekundu wa Msimbazi hao walipokea kipigo kama hicho kabla ya dakika 30 za nyongeza kumalizika na kuingia kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti na Simba kushinda 3-2, hivyo kutinga hatua ya makundi.

Hivyo, ushindi wa bao 1-0 iliyoupata Jumamosi dhidi ya Wydad, ambao ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo, unaifanya Simba kuamini inaweza kwenda kuonyesha maajabu Morocco kama ilivyofanya mwaka 2003 nchini Misri dhidi ya Zamalek.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji wanaendelea na maandalizi kuelekea mechi yao ya marudiano na watakuwa tofauti kabisa Jumamosi wiki hii watakaposhuka katika Uwanja wa Mohammed V nchini Morocco dhidi ya Wydad.

"Tunaitaka nusu fainali, tunaenda kuiona Simba ya tofauti katika Uwanja wa Mohammed wa Tano, kwa sababu wachezaji nao wanaitaka hii mechi na kila moja anacheza kwa moyo.

"Tunaenda kumvua ubingwa Wydad Casablanca, tunaenda kumfanyia balaa kubwa katika uwanja wao wa nyumbani, ukizingatia Jean Baleke analifahamu vizuri dimba hilo," alisema Ahmed.

Aliongeza Robertinho akisaidiana na Juma (Mgunda) wanaendelea kukinoa kikosi

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >